Nipashe
Jumanne Februari 27, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581599
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
Maoni@guardian.co.tz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**SERIKALI** yaondoa hofu tetesi za Bwawa Nyerere kubomoka kingo

UKURASA 3

**MIAKA 3 YA SAMIA** Ngorongoro yenye kicheko, watalii kibao, mapato serikalini yamea



UKURASA 4

**TRENI** ya umeme rasmi katika reli, majaribio kabla ya safari yaanza

UKURASA 5



**BENCHIKHA ACHORA RAMANI YA KUIMALIZA JWANENG GALAXY**

UKURASA 24

UKURASA 2

## MAZISHI WATU 25

# RC aita bodaboda, daladala uwanjani



## Fasheni mpya uuzaji sukari kwa foleni, ukomo idadi kilo

UKURASA 2

Baadhi ya wafanyabiashara katika Manispaa ya Morogoro wakipanga foleni kwenye moja ya maduka ya jumla yaliyoko eneo la Juwata jana ili kupata sukari ambayo imeadimika. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

UKURASA WA 7

## JOTO LATESA WAKAZI, BINGWA WA MUHIMBILI ATAJA MBINU KULIKABILI

JOTO limekuwa kali Dar es Salaam, wakazi wake wanalalama huku Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ikitangaza litakuwa kali...

UKURASA WA 19

## MAUAJI GAZA YAMCHOMOA WAZIRI MKUU PALESTINA

WAZIRI Mkuu wa Palestina, Mohammad Shtayyeh, amejiuzulu kutokana na kushamiri kwa ghasia katika eneo la Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kwa mabavu na Israel na kuendelea kwa vita vinavyosababisha mauaji ya halaiki huko Ukanda wa Gaza...

## 'Maandamano ya CHADEMA rukhsa leo, tutawalinda'

UKURASA 3

**MICHEZO** GUEDE AAHIDI MOTO ZAIDI YANGA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua moja ya darasa la awali katika Shule ya Msingi Sabasita iliyopo Bunda mkoani Mara, akiwa kwenye ziara yake mkoani humo jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

MAZISHI YA WATU 25

# RC aita bodaboda, daladala uwanjani

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, ameomba ushirikiano wa wakazi wa mkoa huo, waendeshaji bodaboda na daladala kuwa sehemu ya umma katika mazishi ya kitaifa ya watu 25 waliofariki dunia katika ajali ya magari manne mwishoni mwa wiki.

Sambamba na hilo, ametangaza kuwapo maandalizi yaliyojitosheleza kiusalama katika kutimiza safari yao ya mwisho ya watu hao.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jini hapa jana, Mongella aliomba wadau wa usafirishaji wa abiria; madereva daladala, bodaboda, bajaji na wananchi wote kwenye jamii, kushiriki na kutoa heshima za mwisho.

Watu hao walifariki dunia katika ajali ya barabarani iliyotokea Jumamosi wilayani Arumeru. Mazishi ya kitaifa yametangazwa kufanyika leo kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha.

Mongella alitangaza jana kuwa shughuli za kuaga miili ya waliofariki dunia katika ajali hiyo iliyotokea eneo la Kibaoni Bypass, Ngaramtoni ya Juu, Barabara Kuu ya Namanga/Arusha, inaanza leo saa 3:00 asubuhi.

"Wananchi wa Arusha, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, kutakuwa na shughuli ya kutoa heshima za mwisho, kwa ndugu zetu. Sasa wanakwenda kupumzishwa. Niwaombe wana-Arusha tushirikiane katika kutoa heshima za mwisho," alisema Mongella.

Kwa mujibu wa Mongella, Rais Samia Suluhu Hassan, alitoa salamu za pole na kutoa maelekezo, namna ya serikali itakavyoghara-mia maziko.

"Kwa hiyo, serikali tunahusika sana na leo katika msiba huu," alisema Mongella.

Ajali hiyo iliyotokea Februari 24, mwaka huu, saa 11 jioni, ikihusisha lori la mizigo lenye namba za usajili KAC 943H aina ya Mack, lenye tela namba ZF 6778, mali ya Kampuni ya KAY Construction ya Nairobi, Kenya.

Uchunguzi wa awali ulibaini lori hilo, lilifeli breki na kuyagonga magari mengine matatu.

Magari mengine yaliyohusika katika ajali hiyo, ni Nissan Caravan, ambalo lilikuwa ni daladala, lenye namba T.623 CQF, gari dogo aina ya Mercedes Benz (Saloon) lenye namba T.879 DBY lililokuwa limewabeba maharusi watarajiwa na wapambe wao.

Pia lilikuwapo basi aina ya Toyota Coaster lenye namba T.673 DEW lililokuwa limebeba raia wa kigeni na baadhi ya wafanyakazi wa Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya New Vision.

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, waliofariki dunia katika ajali hiyo ni wanamume 14 na wanawake 10 na mtoto mdogo wa kike.

Kati ya waliofariki, wamo raia saba wa kigeni waliokuwa wamepanda basi la shule.

***Imeandikwa na Cynthia Mwilolezi na Godfrey Mushi (Arusha)**

# Fasheni mpya uuzaji sukari kwa foleni, ukomo idadi kilo

**Na Waandishi Wetu**

UPATIKANAJI wa sukari bado kitendawili. Katika baadhi ya maeneo kumeendelea kushuhudiwa mtindo wa kupanga foleni ili kuipata kwenye maghala ya wasambazaji wakubwa.

Jijini Dar es Salaam jana, kwenye baadhi ya maduka ya mtaani ilikuwa inauzwa kati ya Sh. 3,000 na 6,000 kwa kilo huku duka la kisasa la Mlimani City ikiuzwa kwa Sh. 3,000, lakini kukawa na masharti; mnunuzi anatakiwa kununua kilo moja pekee.

Agness John, mkazi wa Kigamboni alisema katika mtaa wake upatikanaji wa sukari ni wa tabu, hali iliyosababisha watoto wake kwenda shule bila kunywa chai jana.

Alisema alipata sukari jana mchana baada ya jirani yake kumshirikisha kuwa wanamwagiza mtu kutoka Zanzibar, hivyo wakachanga kila mmoja akaagiza kilo tano.

Steven Shayo, mkazi wa Oysterbay, jijini, alisema upatikanaji sukari umekuwa mgumu hadi kwenye maduka makubwa ya kisasa (supermarkets) kuamua kuuza kilo moja kwa kila mteja ili watoe huduma kwa watu wengi.

"Jana nilikwenda Mlimani City, nikakuta imebaki mifuko miwili ya kilo moja moja, nikaibeba yote, kufika sehemu ya kulipia, nikaambiwa kuwa utaratibu mpya ni kuwa kila mteja anaruhusiwa kununua kilo moja tu ya sukari ili angalau wateja wengi wapate," alidai.

Ashura Rajab, mkazi wa Tabata alisema uhaba wa sukari umefanya baadhi ya maduka kuuza bidhaa hiyo kwa kuangalia mahitaji yako, akitolea mfano kuwa alikwenda dukani akiwa na mteja mwingine na mwenye duka aliamua kumwuzia mwenzake kwa sababu alikuwa amebeba mtoto.

**MOROGORO**

Jana kulishuhudiwa wafanyabiashara wa maduka ya bidhaa za rejereja wakipanga foleni kununua sukari kwenye moja ya maduka ya jumla yaliyoko eneo la Nunge, baadhi wakidai foleni hiyo ilifanya wakumbuke enzi za uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Hamida Juma, mmoja wa wafanyabiashara hao, alidai amelazimika kupanga foleni kuanzia saa moja asubuhi hadi saa sita mchana kwenye duka walioambiwa lina sukari.

"Tukienda kwenye maduka ya jumla tuliyoyazoea, tunaambiwa 'sukari hakuna', tumeikuta hapa kwa wakala Hassan Nzoo na hiyo inaonesha kana kwamba ni maduka ya ushirika ya enzi ya Nyerere yamerudi lakini kama ndivyo, basi maduka ya ushirika yangekuwa mengi," alilalama.

Edina Kajembe, mfanyabiashara mwingine aliyekuwa amepanga foleni katika duka hilo, alishauri serikali ihakikishe viwanda vya sukari vinatoa sukari ya kutosha ili wananchi wapate sukari bila tatizo wala usumbufu wanaoupata kwa sasa.

Mfanyabiashara mwingine, Faraji Hussein alisema kwa sasa mjini Morogoro wapata sukari kwenye maduka madogo kwa bei ya Sh. 110,000 hadi 120,000 kwa mfuko wa kilo 25 huku wauzaji wakichagua wa kuwauzia bila kuwapa risiti.

Muuzaji wa duka hilo la jumla ambaye hakutaka kutaja jina lake, alisema sukari kwenye maduka ya jumla inauzwa Sh. 70,000 kwa mfuko wa kilo 25 huku kilogramu 50 ikiuzwa kwa Sh. 140,000.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari Ikulu, Dar es Salaam wiki iliyopita, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliwataka wananchi kuvumilia wakati serikali inachukua hatua mbalimbali ikiwamo kuagiza bidhaa hiyo kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) baada ya wenye viwanda kupewa vibali na kushindwa kutekeleza.

Alisema wenye viwanda wana hiyari ya kuchagua wauze sukari kama inavyotakiwa au waache kufanya biashara hiyo. Serikali imewalinda kwa zaidi ya miaka 20 na sasa itapeleka muswada wa mabadiliko ya sheria bungeni ili soko liwe huru nao washindane huku wakiwekewa motisha kama wawekezaji wengine.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari Tanzania, Prof. Kenneth Bengesi, alisema mahitaji ya sukari ya kawaida ni tani 552,000 huku hali ya uzalishaji ni tani 445,000 na kuwa na upungufu wa tani 200,000. Viwandani mahitaji ni tani 255,000 ambazo hazipo.

***Imeandikwa na Jenifar Gilla (DAR) na Christina Haule (MOROGORO)**

# Serikali yaondoa hofu tetesi za Bwawa Nyerere kubomoka kingo

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imewahakikishia wananchi kuwa ujenzi wa mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JHPP) umezingatia viwango vya juu vya ubora na lina uwezo wa kuhimili mvua kubwa.

Akiwasilisha taarifa ya mradi kwa ugeni wa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhandisi wa mradi huo, Lutengano Mwandamo, alisema juzi kuwa wamefanya makadirio ya kuona hali ya hewa kwa miaka mingi na ikiwa juu na chini.

Wamebaini kuwa miaka 10,000 inaweza kuchukua maji yanayotiririka kiasi cha mita za ujazo 83.3 kwa sekunde ambayo miundombinu iliyoko kwenye bwawa inamudu.

"Bado tupo salama kwa kiasi cha maji kinachokuja na matarajio ya maji mengi zaidi. Tunatumia taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ambazo zimetuonesha tunaweza kuhimili na hata kuruhusiwa kupita yatapita," alisema.

Kuhusu ukosefu wa maji, alisema mradi umejengwa kwenye Bonde la Mto Rufiji lenye vyanzo vingi vya maji na uwezekano kwamba litasimama kabisa maji yasitiririke haitatokea. Kwa kiwango cha maji kilichopo, uzalishaji unaweza kuendelea kwa mwaka mmoja na nusu bila maji mapya kuingia.

Mwandamo alisema waliangalia historia ya miaka mingi na kuonekana eneo lenye chanzo, maji yako kiasi gani na kufikia uamuzi wa kujenga bwawa hilo na kwamba matengenezo hayatafanyika kwa wakati mmoja, bali yatapishana kutoka kinu cha kwanza hadi cha tisa.

Mkurugenzi wa TANESCO, Gissima Nyamo-Hanga alisema kuna mpango mwingine nje ya umeme kutoka kwenye bwawa hilo kutoka vyanzo vya gesi, maji na nishati mbadala vinavyozalisha megawatt 1,935.

Pia kuna miradi ya vyanzo vipya ikiwamo kutumia ushoroba wa bomba la mafuta la Hoima kwa kuzalisha gesi. Lengo ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2035 uzalishaji umeme nchini unafikia megawatt 10,000.

"Kuhusu kukatika kwa umeme, ni kweli kabisa hii ni kutokana na kuongezeka mahitaji ya umeme, kuna maeneo yanazidiwa.

"Tangu Januari tumekuja na mpango wa kuufungua Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuangalia laini zenye watumiaji wengi na kuongeza huduma ili kuendana na ukuaji wa haraka wa shughuli za kila siku.

"Tutaendelea kupambana, umeme ni biashara yetu ndio maana kila siku tutaendele kuboresha kuhakikisha huduma bora inapatikana kwa wananchi," alisema.

Akizungumza na ugeni huo uliojumuisha wahariri wa vyombo vya habari, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko alisema kuanzia sasa wananchi wanaoishi jirani na vyanzo vya umeme watapewa nishati hiyo na kutokuwa kwenye ratiba ya mgawo.

Alisema walitembelea Mtwara na Lindi na kukuta wana shida ya umeme na serikali imetatua kwa kupeleka mtambo wa megawatt 20 ambao utafungwa kwa ajili ya kulisha mikoa hiyo.

Kwa mujibu wa Dk. Biteko, kuanza kutumika umeme wa JHPP ni likizo isiyozidi miaka 15 inayoitaka nchi kuwa na mpango wa vyanzo vipya vya umeme na kuimarisha vilivyopo.

Alisema anatarajia kupeleka waraka kwenye Baraza la Mawaziri kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa gesi utakaozalisha megawatt 700.

# 'Maandamano ya CHADEMA rukhsa Arusha, tutayalinda'

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) leo kinahitimisha maandamano yake jijini Arusha ikiwa ni takribani siku 33 tangu kilipoanza kuandamana katika majiji Januari 24, mwaka huu.

Vilevile, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, amesema serikali inatambua kuwapo maandamano hayo na itahakikisha wanaandamanaji wanalindwa na Jeshi la Polisi kwa mujibu wa sheria.

Maandamano hayo yanayoongozwa na viongozi wa kitaifa, akiwamo Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, yanalenga kushinikiza serikali kuondoa bungeni miswada mitatu ukiwamo wa mabadiliko ya sheria za uchaguzi, kuboresha katiba mpya na mambo mengine.

Katibu wa chama hicho Kanda ya Kaskazini, Amani Golugwa, alisema jana jijini Arusha kuwa maandalizi yote ya maandamano jijini humo yamekamilika.

"Sisi kama chama, tunahuzunika na waliopata msiba huu mzito na tumetoa pole kwa wafiwa. Isipokuwa watu wanatakiwa kufahamu jambo moja kwamba:

"'Urban Setting' (mandhari ya mjini) inaruhusu mchanganyiko wa mambo kufanyika kwa wakati mmoja, iwe kuendelea na shughuli za gulio, siasa au kusherehekea mambo ya soka, bila ya kuathiri utamaduni, mazoea au mila zetu.

"Tunaomboleza nao waliopata msiba, lakini hatuwezi kusimamisha mambo. Hivi sasa tunaendelea na maandalizi kama kawaida," alisema Golugwa, akihusisha maandamano yao na mazishi ya kitaifa ya watu watano waliofariki dunia kutokana na ajali iliyohusisha magari manne jijini Arusha mwishoni mwa wiki.

Alisema maandamano hayo pia yanalenga kusukuma serikali kuja na mpango wa dharura wa kukwamua wananchi dhidi ya makali ya maisha wanayopitia kwa sasa.

Akizungumzia maandamano hayo jana, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mongella alisema: "Kwa ushauri wa wadau wa Arusha, mimi niseme, si kwamba ninaomba, isije ikapotoshwa, si kwamba hatutambui kuwapo maandamano.

"Ratiba ya maandamano, ipo palepale na ipo kisheria na mifumo yote ya kiserikali, itahakikisha maandamano yanakuwa salama, kama yalivyosimamiwa maeneo mengine naomba hilo lieleweke."

Mongela aliendelea kufafanua kwamba: "Lakini ninyi mnajua, hata kwenye jamii zetu si jambo zuri, lakini misiba inatokea na wakati mwingine mmeshapanga harusi siku ya mwisho msiba unatokea.

"Sasa mnafanyaje hapana? Kuna watu wanaweza kutafuta jibu la haraka, tunaahirisha harusi na kuna mahari watu wameshatoa na mmeshakula."

Kuhusu usalama, Mkuu huyo wa Mkoa, alisema serikali itahakikisha maandamano hayo yanalindwa na kufanyika kama yalivyopangwa.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
27/02/2024

## TAARIFA KWA UMMA

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe **28/02/2024** kampuni ya **AFRICA WAKAWAKA LOGISTICS CO. LTD** itasafirisha mzigo mkubwa kutoka **Dar es Salaam** kuelekea **Rusumo** kupitia **Dodoma.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**1.T 102 EFR / T 747 ECA**
**2. T 106 EFR / T 992 EBX**

VIPIMO
**Urefu - 22m** **Upana - 4.7m,** **Kimo - 5.0**

Gari litasafirisha mzigo kuanzia saa **12:30 Asubuhi** mpaka saa **12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwanga Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | NYARAKA YA UMILIKI NA SEHEMU | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | UPENDO GODWIN LEMA | GARI | T683 DCS- NISSAN DUALIS | JODAC PROFESSIONAL LTD | 05/03/2024 |
| 2 | ANDULILE GREEN JAMES | GARI | T328 DQU – DAF TRUCKS | JODAC PROFESSIONAL LTD | 05/03/2024 |
| 3 | RINGSON VICENT MBERESERO | GARI | T 971 DPL –SUZUKI ESCUDO | JODAC PROFESSIONAL LTD | 05/03/2024 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**
- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

DRC Danish Refugee Council
P.O Box 177
Old IRC Road
Kibondo, Kigoma
Tanzania
T: +255 282 820 163
EAGL-info@drc.ngo
www.drc.ngo

DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

## TANGAZO LA ZABUNI

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISH LINATARAJIA KUINGIA MKATABA WA HUDUMA MBALIMBALI KAMA IFUATAVYO;
- UGAVI NA UTOAJI WA VIFAA VYA MATIBABU
- UGAVI NA UTOAJI WA VIFAA VYA KOMPUTA
- UGAVI NA UTOAJI WA VITU VYA USAIDIZI WA MSINGI (KUJIKIMU)
- UTOAJI WA HUDUMA ZA UKODISHAJI WA MAGARI
- UTOAJI WA HUDUMA ZA TAXI (DAR ES SALAAM PEKEE)
- UTOAJI WA HUDUMA ZA UKARABATI/MATENGENEZO YA MAGARI
- UTOAJI WA HUDUMA ZA UPISHI
- UTOAJI WA HUDUMA YA SAFARI NA TIKETI ZA NDEGE

HIVYO SHIRIKA LA DANISH LINATANGAZA ZABUNI TAJWA HAPO JUU NA WAZABUNI WAFUATE MAELEKEZO YAFUATAYO.
- USITUMIE WINO WA MAJI KUSAHIHISHA UNAPOFANYA KOSA.TUMIA KARATASI MPYA
- USIBADILISHE KARATASI ZA ZABUNI KWENDA KWENYE MFUMO WORD/EXCEL,
- ZINGATIA SEHEMU ZA KUSAINI NA KUGONGA MUHURI AMBAZO NI LAZIMA
- USISAHAU KUAMBATANISHA NYARAKA ZINAZOHITAJIKA KAMA ZILIVYOAINISHWA. BAADA YA KUMALIZA SEHEMU ZOTE SAINI, GONGA MUHURI, WEKA TAREHE.

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAALIKA WAZABUNI KUWASILISHA MAOMBI YAO YA UZABUNI.

NYARAKA HUSIKA ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 27.02.2024 HADI TAREHE 11.03.2024 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

MWISHO WA KURUDISHA ZABUNI NI TAREHE 11.03.2024 SAA 10:00 JIONI

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA +255 653 468 638 au BARUA PEPE **joram.nshatsi@drc.ngo**

**UNAPASWA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA BARUA PEPE: rfq.tza@drc.ngo AU KULETA MOJA KWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.**

MIAKA MITATU YA SAMIA

# Kicheko chatawala Ngorongoro watalii, mapato yakiongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

IDADI ya watalii wanaotembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) imeongezeka sambamba na mapato yatokanayo na wageni hao.

Imebainishwa na uongozi wa mamlaka hiyo uliojawa tabasamu kwamba, kwa mwaka 2022/23, idadi ya wageni wanaotembelea NCAA ilikuwa 752,232 kulinganishwa na wageni 191,614 waliotembelea hifadhi hiyo mwaka 2020/21.

Kamshina Mkuu wa NCAA, Richard Kiza alibainisha hayo alipozungumza na wahariri na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mafanikio ambayo mamlaka hiyo imepata katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Kamishna Kiza alisema hayo ni miongoni mwa mafanikio ambayo mamlaka hiyo imepata kwa kipindi hicho, ikisifu jitihada zilizofanywa na Rais Samia kuinua sekta ya utalii na uhifadhi tangu aingie madarakani Machi 19, 2021.

Alisema NCAA inatarajia kuongeza idadi ya watalii hadi kufikia milioni moja katika mwaka huu wa fedha (2023/24) na kuiongezea serikali mapato.

Tangu Julai 2020, mapato ya utalii nchini yanakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hivyo kupelekwa hazina. Awali yalikusanywa na mamlaka za uhifadhi; Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), NCAA na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA).

Kamishna Kiza alisema kutokana na jitihada za serikali chini ya Rais Samia, NCAA sasa inapata fedha kwa wakati na kufanya ufuatiliaji wa huduma zinazotolewa kwa wageni.

Alisema kutokana na ongezeko hilo la watalii, ukusanyaji wa mapato, unatarajia kuongezeka hadi kufikia Sh. bilioni 200 kwa mwaka huu wa fedha.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia madarakani, mamlaka hiyo imepata mafanikio makubwa katika shughuli zake za kila siku.

Alisema kuwa Rais Samia amekuwa chachu ya maendeleo ya mamlaka hiyo kutokana na kushiriki kwake katika filamu ya Tanzania The Royal Tour ambayo imesaidia kwa kiwango kikubwa kuongeza idadi ya watalii wanaofika kutembelea hifadhi.

"Juhudi za Rais Samia katika kukuza utalii hazikuishia tu kwenye filamu ya Tanzania The Royal Tour bali pia katika kuhakikisha mamlaka inapata fedha za uendeshaji kwa wakati, jambo ambalo limesaidia kulipa mishahara pamoja na stahiki nyingine za watumishi kwa wakati, kujenga miundombinu ya ofisi, barabara, maji na umeme na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kuona huduma zinazotolewa kwa watalii zinakuwa za kisasa na zisizo na usumbufu," alisema.

Kamishna Kiza alisema kuwa wakati Rais Samia anaingia madarakani Machi 19, 2021, alikuta sekta ya utalii ikiwa na hali mbaya kiasi kwamba idadi ya wageni ilishuka, lakini kutokana na maono yake na juhudi zake binafsi katika kipindi cha miaka mitatu ya serikali yake, mamlaka imeshuhudia mambo makubwa.

Alisema katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, hifadhi hiyo imepokea wageni 534,065, likiwa ni ongezeko la asilimia 10 kulinganishwa na idadi ya wageni waliotembelea hifadhi katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23.



Kuhusu mapato yatokanayo na utalii, Kamishna Kiza alisema yameongezeka kutoka Sh. bilioni 31 mwaka 2020/21 hadi kufikia Sh. bilioni 171 mwaka 2022/23.

"Hiki ni kiwango cha juu zaidi kuwahi kukusanywa na mamlaka. Mapato yanatarajiwa kuongezeka zaidi na kufikia takribani Sh. bilioni 200 kwa mwaka kwani katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, Sh. bilioni 123 zimekusanywa.

"Mapato haya yameongezeka kwa asilimia 13 kulinganisha na mapato yaliyokusanywa katika kipindi hicho hicho mwaka 2022/23," alibainisha.

Kamishna huyo wa uhifadhi pia alisema kuwa mbali na kutangaza Tanzania kupitia filamu maarufu ya Tanzania The Royal Tour, Rais aliagiza NCAA ipatiwe fedha za mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19 Sh. bilioni 6.645 ambazo zilitumika kuimarisha miundombinu ya barabara na kununua mitambo pamoja magari makubwa ya kutengenezea barabara.

Alisema kuwa fedha hizo pia zilitumika kuimarisha viwanja vya ndege pamoja na miundombinu mingine ya utalii ili wageni wavifikie vivutio vya utalii kwa urahisi.

Alisema serikali pia imetenga Sh. bilioni 69 kwa ajili ya kujenga tabaka gumu kipande cha barabara chenye urefu wa kilomita 29.5 kutoka lango kuu la kuingilia NCAA hadi Seneto.

Alisema Novemba mwaka 2022, Rais Samia alifanya ziara ya kikazi China na kupata Sh. bilioni 25 kwa ajili ya kuendeleza Ngorongoro Lengai UNESCO Geopark pamoja na miundombinu mingine ya utalii ikiwamo nyumba ya makumbusho itakayojengwa katika lango kuu la kuingilia Ngorongoro.

Kamishna Kiza alitaja mafanikio mengine waliyopata katika miaka mitatu ya Rais Samia madarakani yanajumuisha kudhibiti ujangili wa tembo kwa kuimarisha ulinzi ndani na nje ya hifadhi, huku wakishuhudia ongezeko la faru kwa asilimia 25. NCAA inamiliki asilimia 25 ya faru weusi waliopo nchini.

Kiongozi huyo wa NCAA pia alitoa ufafanuzi kuhusu uamuzi wa serikali kuhamisha wananchi na mifugo ndani ya hifadhi hiyo, akieleza madhara ya kiikolojia ya ongezeko la watu na mifugo hifadhini.

Alisema kuwa wakati NCAA inaanzishwa mwaka 1959, kulikuwa na wananchi wasiozidi 8,000. Kati yao, 4,000 ni waliokuwa Ngorongoro na 4,000 walihamia kutoka Hifadhi ya Taifa Serengeti.

Alisema kuwa kipindi hicho idadi ya mifugo ya wananchi wakati huo ilikuwa takribani 261,000.

Hali hiyo ni tofauti na miaka ya hivi karibuni. Kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu nchini (NBS), wananchi katika Tarafa ya Ngorongoro wameongezeka kutoka 8,000 mwaka 1959 hadi kufikia zaidi ya watu 100,000 na mifugo ikiongezeka kufikia zaidi ya 850,000 (Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022). Eneo hilo lina ukubwa wa kilomita za mraba 8,292.

**KUHUSU NCAA**

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ilianzishwa kwa Sheria Na. 413 ya Mwaka 1959 kwa kuigawa Hifadhi ya Taifa Serengeti (SENAPA), ili kuanzisha hifadhi yenye upekee duniani; ina wanyamapori, mifugo na binadamu.

Kamishna Kiza aliyataja mambo yaliyosababisha hifadhi hiyo kugawanywa kuwa ni kuendeleza uhifadhi wa maliasili na malikale, kusimamia maendeleo ya jamii ya watu wanaoishi ndani ya mamlaka Wahdzabe, Masai, Datoga na kuendeleza utalii.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 26 FEB' 2024

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMANNE tarehe 27 FEB 2024 kampuni ya TRANSCARGO LTD itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA, gari hilo lenye namba za usajili: T762CPQ/T964EBA/T965EBA.

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 22.50
Upana - mita 4.20
Kimo - mita 4.60

3. Njia itakayotumika: DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA Kupitia MOROGORO gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.


## Majaliwa: Samia ni kinara utekelezaji ilani ya CCM

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Kassim Majaliwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ni kinara katika utekelezaji ilani ya chama hicho.

Aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano Mkuu wa CCM Jimbo la Kavuu uliofanyika katika Shule ya Sekondari Mizengo Pinda, Halmashauri ya Mpimbwe, Wilaya ya Mlele, mkoani Katavi.

"Ni ukweli usiopingika kuwa Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais na Mwenyekiti wa chama chetu amekuwa kielelezo cha mafanikio makubwa yanayofikiwa na nchi yetu kwa sasa," alisema.

Majaliwa alisema kuwa tangu Rais Samia ashike madaraka hayo, ameendelea kutekeleza miradi yote ya kimkakati kama ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 ilivyoelekeza.

"Dk. Samia ameendelea kusimamia utekelezaji ilani ya CCM ikiwamo upatikanaji huduma za afya kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa, kanda na rufani," alisema.

Waziri Mkuu alisema pamoja na mafanikio mengine, Rais Samia ameimarisha diplomasia ya kiuchumi na nchi mbalimbali sambamba na kukuza utalii, lugha ya Kiswahili na masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi.

"Taifa hili, chini ya serikali za CCM tuna uwezo mkubwa wa kujitegemea na kujiletea maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii.

"Haya yamedhihirika kupitia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika ujenzi wa taifa letu na kuboresha maisha ya Watanzania katika nyanja mbalimbali," alisema.

Majaliwa alisema CCM imekuwa nguzo ya amani, umoja na mshikamano miongoni mwa Watanzania na hivyo kuwa chachu ya maendeleo nchini.

"Umuhimu wa chama chetu umeendelea kuonekana kwa jinsi ambavyo kimekuwa kikitumikia Watanzania huku nchi yetu ikidumisha umoja na amani miongoni mwa wananchi," alisema.

Mbunge wa Kavuu ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geoffrey Pinda, alisema jimbo hilo na Halmashauri ya Mpimbwe kwa ujumla wamepiga hatua kubwa katika utekelezaji ilani ya CCM kwenye sekta za afya, elimu, miundombinu na maendeleo ya jamii.

Alisema kuwa zaidi ya Sh. bilioni 1.2 zimetolewa kugharamia elimu bila malipo na Sh. milioni 238 zimetumika kukarabati shule kongwe.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, alisema Sh. bilioni 800 zimepokewa kwa ajili ya utekelezaji ilani ya CCM na kuahidi wataendelea kusimamia ilani hiyo pamoja na fedha zinazoletwa na serikali kutekeleza miradi mbalimbali.

Akiwa njiani kuelekea Mpimbwe, Majaliwa alisimama na kuzungumza na wananchi wa eneo la Sitalike ambako pamoja na mambo mengine, amewaomba wawe wavumilivu wakati serikali ikiendelea kutatua mgogoro wa ardhi katika eneo hilo.

HABARI KITAIFA



Waliokuwa walinzi wa Kampuni ya Ulinzi ya Security Group of Afrika (SGA) wanaokabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi na wizi wa fedha zaidi ya Sh. milioni 780 wakitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana baada ya kuhukumiwa miaka miwili jela na mali zao zote kutaifishwa kuwa mali ya serikali. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Treni za umeme kuanza rasmi Julai

**Na Jenifer Gilla**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limesema treni za umeme zitaanza kutoa huduma ya usafiri kuanzia mwezi Julai, mwaka huu, likiwatoa hofu Watanzania kuhusiana na kukatika kwa umeme wakati zikiwa safarini. Katika majaribio ya treni hizo kwa safari za kutoka Mkoa wa Dar es Salaam hadi Morogoro kupitia njia ya Pugu jana, Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alisema kuanza kwa safari hiyo ni utekelezaji wa agizo alilotoa Rais Samia ili kuboresha na kurahisisha huduma ya usafiri kwa wananchi.

Alisema wanategemea kuwa mwezi ujao wataanza majaribio ya treni hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, huku akimshukuru Rais Samia kwa jitihada alizofanya kuhakikisha mradi huo unafanikiwa na kufikia hatua ya majaribio.

Kadogosa aliwatoa hofu Watanzania kuhusu kukatika umeme wakati treni zikiwa safarini, hivyo kusitisha safari, kwa kuwa ina treni hizo zinatumia umeme kidogo pia kuna transfoma zenye uwezo wa kupunguza umeme.

Alisema treni hizo pia zimetengenezwa kwa mfumo ambao unaweza kutumia umeme na dizeli, hivyo inapotokea umeme ukakatika, zina uwezo wa kujibadilisha na kutumia mafuta bila hata abiria kugundua.

"Kwa sasa hivi Watanzania wasiwe na wasiwasi wowote kwamba 'treni hiyo inaweza kuzimika katikati kule tukapata shida', hicho kitu hakitatokea," alisema.

Kadogosa alisema abiria akiwa ndani ya usafiri huo atapata huduma mbalimbali muhimu ikiwamo choo, kuchaji simu na kompyuta mpakato, intaneti na mazingira mazuri ya kufanya kazi binafsi au vikao kwa wale watakaohitaji huduma hiyo.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alisema kupitia treni hiyo, Tanzania inajiwekea historia ya kuwa nchi pekee Afrika Mashariki na Kati kuwa na treni ya umeme ambayo ni fursa nzuri ya kutoa huduma hadi nchi za jirani.

Alishauri wafanyabiashara wanaotumia njia inayopita treni hiyo kutumia fursa ya kuwapo usafiri huo kuokoa muda wanapokwenda katika maeneo hayo kwa ajili ya shughuli zao kwa kuwa inatumia muda mfupi kulinganisha na usafiri wa basi.

Alisema treni hiyo ina ubora sawa na zile zilizopo kwenye nchi zilizoendelea, zikiwamo za mabara ya Asia, Amerika na Ulaya, hivyo Watanzania wanapaswa kujivunia kwa hilo.

Desemba 31, mwaka jana, Rais Samia aliielekeza Wizara ya Uchukuzi kuhakikisha kuwa ifikapo mwisho mwa Julai, mwaka huu treni za umeme zianze kutoa huduma kwa wasafiri kati ya Dar es Salaam na Dodoma.

Alisema amekuwa akisikia kuwapo mabadiliko ya tarehe za kuanza kwa safari hizo huku wananchi wakichoshwa na sababu zinazotolewa kila mara kuhusiana na mabadiliko hayo.

# 'Tumieni mfumo mpya wa EPZA kujitanua kibiashara'

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji wa Mauzo Nje ya Nchi (EPZA) imehimiza wawekezaji nchini kutumia mfumo mpya wa kidigitali wa mamlaka hiyo ili kuhuisha taarifa zao kama fursa muhimu ya kujitanua zaidi kibiashara.

Mwaka jana, EPZA ilizindua mfumo mpya wa kidigitali wa kuhudumia wawekezaji (EPZA Business Facilitation Portal) ili kuweza kuwafikia na kuwapa huduma wawekezaji kwa urahisi na ufanisi zaidi.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi wa EPZA, William Msoffe, alitoa rai kwa wawekezaji kutumia mfumo huo wakati wa ziara ya kutembelea viwanda vilivyo chini ya EPZA katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma mwishoni mwa wiki.

"Mfumo huu ni fursa muhimu sana kwa wawekezaji kupata taarifa sahihi na kwa haraka kutoka kwenye mamlaka ya EPZA na pia katika kujipanua zaidi kibiashara," alisema.

Aliongeza kuwa wawekezaji wote waliotembelewa walisisitizwa kuhuisha taarifa zao kwa kutumia mfumo mpya wa kidigitali uliojengwa na mamlaka ambapo kwa kufanya hivyo, utoaji leseni kwa wawekezaji wanaotaka kuwekeza chini ya EPZA umerahisishwa.

Mamlaka ya EPZA imefanya tathmini ya viwanda vyake vilivyoko Nyanda za Juu Kusini kwa lengo la kutathmini viwanda vilivyo chini yake nchi nzima.

Alisema katika ziara hiyo ya Nyanda za Juu Kusini, walitembelea viwanda saba katika Mkoa wa Lindi, viwanda 10 katika Mkoa wa Mtwara na eneo maalum la kiuchumi kwa ajili ya uzalishaji bidhaa za kuuza nje ya nchi (SEZ) mkoani Ruvuma.

Msoffe alisema ziara hiyo ililenga kuangalia maendeleo ya wawekezaji, kuboresha taarifa za wawekezaji na kupokea changamoto zinazokabili wawekezaji hao ambao ni zaidi ya 200 kwa nchi nzima.

Lengo lingine la ziara hiyo ni kutoa elimu kuhusu programu za EPZ na SEZ kwa wadau mbalimbali.

Alisema elimu iliyotolewa wakati wa ziara hiyo ni kuhusu EPZ na SEZ, malengo ya kisera ya mamlaka, majukumu ya EPZA kisheria na elimu kuhusu vigezo vya uwekezaji katika programu ya EPZ na SEZ.

Pia walitoa elimu ya muundo na bodi ya mamlaka hiyo, elimu kuhusu vivutio vya programu ya EPZ na SEZ, elimu kuhusu matokeo ya uwekezaji tangu mamlaka ianzishwe, elimu kuhusu halmashauri kutenga maeneo ya uwekezaji na elimu kuhusu changamoto za mamlaka.

Alisema tathmini hiyo itaiwezesha mamlaka kutatua changamoto za wawekezaji na hivyo kufikia lengo lake la kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda, ikisaidia kutengeneza ajira, kuongeza ushindani wa malighafi za ndani na kuliongezea taifa fedha za kigeni.

Msoffe pia alisema kwa sasa mamlaka kupitia programu za EPZ SEZ, inazalisha bidhaa ambazo zimekidhi vigezo/viwango vya soko la Marekani, Asia, Ulaya na masoko mengine ndani ya Bara la Afrika.

Bidhaa ambazo zimeshaanza kuuzwa nje kwa kufikia viwango ni bidhaa kutoka sekta za kilimo, madini, nishati, misitu, nguo na vyuma.

hakielimu

CALL FOR CONSULTANCY

To undertake baseline survey of the Accountability for Child Rights Initiative (ACRI)

How to apply

Interested consultants should submit their technical and financial proposals to **procurement@hakielimu.or.tz** not later than 4th March 2024. The ToR is available at **www.hakielimu.or.tz**

www.hakielimu.or.tz info@hakielimu.or.tz @hakielimu

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunaipongeza serikali utekelezaji mradi wa Bwawa la Julius Nyerere

**HATIMAYE** serikali imeingiza megawatt 235 kwenye Gridi ya Taifa ambazo zimepunguza mgawo wa umeme kwa asilimia 85, baada ya kuwasha mtambo namba tisa kati ya idadi hiyo inayowezeshwa jumla ya megawatt 2,115 katika Bwawa la Nyerere.

Ni hatua iliyotangazwa juzi na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, ambaye pia aliahidi kuwa mwezi ujao Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Misri, Abdel-Fatah Alsisi, watazindua mtambo namba nane na hivyo kuwezesha nchi kuwa na megawatt 470 zinazoongezwa kwenye Gridi ya Taifa kutoka mradi wa kufua umeme wa maji wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP).

Kwa mujibu wa Naibu Waziri Mkuu Biteko, kuwashwa kwa mtambo huo kumefanya upatikanaji umeme nchini kuwa wa asilimia 98, mgawo umepungua na utakwisha mwezi ujao.

Nipashe tunapongeza hatua hiyo ya serikali ambayo si tu kwamba inakwenda kutatua kero ya muda mrefu ya mgawo wa umeme nchini, bali pia inaingiza nchi kwenye historia ya utekelezaji wa mradi mkubwa.

Mradi huo wenye thamani ya Sh. trilioni 6.6, ulianza kutekelezwa mwaka 2015 licha ya kuwapo ukosoaji mkubwa ndani ya nje ya mipaka ya Tanzania, uliojikita katika hoja ya athari za kimazingira. Serikali chini ya uongozi wa Rais John Magufuli ilisisitiza kupuuza ukosoaji huo.

Tunapongeza uthubutu huo wa serikali ambao sasa unakwenda kuifanya nchi kuwa na 'utajiri wa umeme'. Kwa mujibu wa Naibu Waziri Mkuu Biteko, upungufu uliokuwapo ni megawatt 200 hadi 400, hivyo kuwashwa kwa mtambo namba tisa kunafanya nchi kuwa na umeme wa ziada megawatt 70, hata kabla ya kuwasha mitambo mingine minane iliyo katika ujenzi.

Serikali inastahili pongezi kwa jitihada zake hizo za kuhakikisha inamaliza kero ya mgawo wa umeme nchini na kuondoa malalamiko miongoni mwa wananchi kwa kukosa nishati ya uhakika.

Pamoja na pongezi hizo, Nipashe tunatambua kwamba mahitaji ya umeme yanaongezeka kila kukicha, hivyo serikali inapaswa kuongeza vyanzo vingine kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana nchini.


Nipashe tunatambua kuwa zipo nchi zilizo na vyanzo vya uhakika vya umeme, lakini kikwazo kikubwa kimekuwa wizi wa umeme unaofanywa na watu wake, maarufu vishoka.

Hivyo, serikali inapaswa kulinda miundombinu ya umeme ili isihujumiwe na watu wachache kwa manufaa yao binafsi na kuhakikisha hakuna wizi wa umeme, ikizingatiwa mradi huo wa Bwawa la Nyerere umetumia fedha nyingi.

Shirika la Umeme (TANESCO) linafanye ukaguzi wa mara kwa mara katika miundombinu ya umeme kwenye maeneo mbalimbali nchini ili kuhakikisha hakufanyiki vitendo vya udanganyifu katika huduma ya umeme kwa wananchi.


Pia elimu itolewe kwa wananchi ili washiriki kulinda miundombinu ya umeme na madhara yanayowezesha kusababishwa na vitendo hivyo.

Tunaipongeza serikali kwa utekelezaji mradi wa Bwawa la Nyerere.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Wafanyabiashara mnawatesa watu

**IKIWA** zimebaki siku chache kabla ya kuanza mfungo wa Ramadhani mwezi ujao, baadhi ya wafanyabiashara wanajiandaa kuvuna kutokana na kupandisha bei ya bidhaa muhimu zinazohitajika.

Ni kawaida katika kipindi cha mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani wafanyabiashara walio wengi hupandisha bidhaa hasa vyakula vinavyotumika sana kuandaa futari.

Vyakula hivyo ni kama ndizi, mihogo, viazi, magimbi, maharage, tambi, unga wa ngano, sukari na tende wakilenga faida kubwa bila kujali kuwa wanawaumiza wanunuzi.

Bei za vyakula zinaongezeka zaidi kutokana na maelezo mengi kwa mfano bei ghali mafuta, kupungua kwa kiwango cha uzalishaji na gharama ya juu ya kuagizia pembejeo kama mbolea na viuatilifu kutoka nje.

Wakati wa mfungo vyakula huuzwa kwa bei ya juu wauzaji wakiamini kuwa ni lazima wateja wawe wengi tena watalazimika kununua hata kama vina bei kubwa kiasi gani.

Ukweli huo unafanana na kutumia fursa wakati au nyakati za sikukuu za kidini wakiamini kuwa ni lazima watu watanunua bidhaa za vyakula.

Na kwenye kufungua shule kadhalika imani ni hiyo kuwa mzazi au mlezi lazima atamnunulia sare, daftari, vitabu na mabagi ya shule ambavyo pia hupandishwa bei mara dufu.

Na kwenye kufungua shule kadhalika imani ni hiyo kuwa mzazi au mlezi lazima atamnunulia sare, daftari, vitabu na mabagi ya shule ambavyo pia hupandishwa bei mara dufu.

Nyakati za kufungua shule watoto au wanafunzi wanahitaji huduma hizo ambazo ni muhimu lakini inafikia hatua zinasababisha maisha ya watu kuwa magumu au kukwama kwani walio wengi wanashindwa kumudu kuhudumia familia.

Mathalani shule zikifunguliwa hapo ndipo mzazi au mlezi anapoanza kutafakari kati ya sare za shule na chakula anaamua kuwa ni bora kula kwani maisha bila chakula hayawezekani na changamoto ya kuongezeka bei vifaa vya shule inasababisha watoto kusubiri au kuacha kusoma.

Hivyo hali hii inachangia wanafunzi wengine kukaa nyumbani wakisubiri wazazi au walezi waweze kupata fedha za kununua mahitaji hayo.

Kwa kiasi kikubwa mambo hayo yanachangia hata kufeli kwa wanafunzi kwani walio wengi hukaa nyumbani kwa kusubiria vifaa hivyo.

Katika nyakati za mwezi Ramadhani kupandisha bei vyakula hili linaonyesha wazi kuwa baadhi ya familia hasa zisizo kuwa na hela zinaweza kukosa vyakula au lishe inayotakiwa kutumiwa na wengi.

Kama walio wengi hula mlo mmoja kwa kawaida au nyakati nyingine wanapata kiasi kidogo cha mlo si hatari zaidi iwapo vyakula vitapanda bei?

Dar es Salaam vyakula vimepanda bei kupindukia kilo ya vitunguu ikiuzwa Shilingi 5,000 wakati reja reja ni Shilingi 500 kwa kimoja. Zipo taarifa kuwa baadhi ya watu wanaagiza sukari Zanzibar inakouzwa Shilingi 3,200 lakini hairuhusiwi kuvuka na zaidi ya kilo tano kutoka Visiwani kuja nazo Bara.

Viungo vingine muhimu kama nyanya nazo ni tishio huuzwa moja 300 pengine tenga limefikia 200,000 na sado ya nyanya ikielekea Sh 8,000. Mchele madukani unanunuliwa kilo Sh. 3,500 hasa ule mzuri siyo chenga, sembe dukani inakaribia Sh. 1,500 hali inazidi kuwa mbaya wakati fungu la mboga linauzwa Shilingi 800 hadi 1,000.

Inakuwa vigumu kununua bidhaa muhimu kuanzia mkaa, kuni na hata mafuta ya taa kwa baadhi ya watu wanaoendelea kutumia nishati hiyo.

Watu walitegemea msimu wa mvua kubwa iliyoanza Novemba hadi Januari mwaka huu ungeleta nafuu lakini mambo sivyo. Bei hazijashuka kwa mazao ya muda mfupi kama vile mboga kabichi ikiuzwa ghali mno. Wakulima katika masoko ya mijini na vijijini wanasema mazao kutoka masoko makuu yameongezeka bei na kuongeza hofu kwa wateja hasa nyakati hizi za sikukuu.

Ni ombi langu kwa serikali iangalie namna kusimamia bei za vyakula kuzuia watu wasiumie kwa sababu wafanyabiashara wanachotaka ni faida wala hawajali maisha ya Watanzania wengi maskini.

**HABARI KITAIFA**

## Daktari Bingwa aonya unene wa kupindukia

Na Joseph Mwendapole

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Dharura katika Hospitali ya Regency jijini Dar es Salaam, Shreya Shah, amewataka Watanzania kupunguza uzito kuendena na urefu wao ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama kisukari na shinikizo la damu.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki huko Gongolamboto, jijini Dar es Salaam baada ya kuendesha upimaji afya kwa wananchi wa Jimbo la Ukonga katika bonanza lililoandaliwa na Mbunge wao, Jery Silaa.

Bingwa huyo alisema kuwa miongoni mwa waliohudhuria upimaji huo wamegundulika kuwa na uzito uliopitiliza, hasa wanawake hali ambayo inawaweka hatarini kupata magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Alisema ni umuhimu wananchi kuelimishwa kuhusu ulaji salama kwa kuepuka matumizi ya kupindukia ya vilevi na vyakula vyenye sukari nyingi, ili kujiepusha na magonjwa kama hayo ambayo yamekuwa yanawapata wananchi wengi.

"Tumeona zaidi ya wananchi 400 na tumebaini wengi wakiwa na uzito mkubwa kuliko urefu wao hasa wanawake, hivyo tumewashauri wafanye mazoezi kila siku na tumewashauri wapunguze matumizi ya mafuta," alisema.

Bingwa huyo aliwataka wananchi kujenga mazoea ya kusikiliza ushauri unaotolewa na wataalamu kuhusu afya, badala ya kusikiliza na kuamini habari za mitaani zinazowapotosha.

Alisema kuwa kwenye upimaji huo, watu wengi waliopimwa hawakukutwa na ugonjwa wa kisukari kwa kuwa wengi wanafanya mazoezi mara kwa mara ya kukimbia.

"Wengi tuliowapima hapa tumewakuta na sukari ya wastani wa 5 na 6 ambayo ni ya kawaida kwa sababu sukari ambayo tunapima na kukuta 7.5 ndiyo tunaanza kuwa na wasiwasi kwamba mgonjwa ana kisukari," alisema Dk. Shah.

Alitaka Watanzania kujenga mazoea ya kufanya mazoezi ya kukimbia kila siku kwa kuwa kwa kufanya hivyo wataepukana na maradhi hayo yasiyo ya kuambukiza.

Alisema hata kama mtu ana matatizo ya mgongo na goti, anaweza kufanya mazoezi mepesi yatakayomsaidia kupunguza uzito, hivyo kujiweka kwenye hali salama kiafya.

"Watu wajitahidi kuacha matumizi makubwa ya mafuta na chumvi nyingi kwa sababu hivi ni hatari sana kwa afya, wawe wanatumia kwa wastani," alisema.

Mmoja wa wananchi waliofika kwenye upimaji huo, Alex Ngomola alisema watu wengi hawana kawaida ya kupima afya zao mpaka wanapokuwa katika hali mbaya.

Alisema hali hiyo wakati mwingine husababishwa na hali ngumu ya kiuchumi, hivyo aliomba hospitali hiyo kuendelea kutoa huduma hiyo ili kuwafikia wananchi wengi ambao hawana uwezo.

"Tunaomba Hospitali ya Regency na wengine waendeleze utamaduni wa kuwa wanapima wananchi afya zao bila malipo angalau mara mbili kwa mwaka kwa sababu wengi wetu kiuchumi hatuko vizuri ingawa tunapenda kupima afya zetu," alisema.

Maria Gwemela aliyehudhuria upimaji huo, pia alitaka watanzania kujenga utamaduni wa kupima afya zao, ili wapate tiba mapema wanapogundulika kuwa na matatizo ya maradhi mbalimbali.

"Tusisubiri upimaji wa bure kama ilivyotokea leo bali tuwe tunakwenda hospitalini kupima angalu mara moja kwa mwaka kwa sababu madaktari wanasema ukibainika una tatizo mapema unatibiwa kwa urahisi kuliko kusubiri hali kuwa mbaya zaidi," alisema.



Balozi wa Norway nchini, Tone Tinned (wa pili kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Kheri James (kushoto), wakimsikiliza Mkurugenzi wa Tiba wa Hospitali ya Haydom, Dk. Pascal Mdoe, walipofanya ziara hospitalini hapo kwa kutembelea mradi mkubwa wa ujenzi wa jengo jipya na kushiriki mijadala ya afya juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Joto latesa wakazi, bingwa wa Muhimbili ataja mbinu kulikabili

Na Christina Mwakangale

JOTO limekuwa kali Dar es Salaam, wakazi wake wanalalama huku Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ikitangaza litakuwa kali zaidi mkoani humo.

Kukiwa na angalizo hilo, Daktari Bingwa wa Mishipa ya Fahamu Ubongo na Misuli katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, Kigocha Okeng'o ametaja hatua za kuchukua kukabili hali hiyo.

TMA ilitangaza juzi kwamba mikoa 10 itakuwa na viwango vya joto kali, kati ya nyuzi joto 34 kwa Dar es Salaam na kiwango cha chini kitakuwa ni kwa mkoa wa Njombe (21).

Dk. Okeng'o ameiambia Nipashe kwamba joto na jua kali vinaweza kuwa sababu ya kipanda uso na kichwa kuuma. "Joto lenyewe linasababisha na, au ni kichocheo cha kichwa kuuma, yaani msongo wa mawazo, harufu kali. Na kwa wanaoumwa zaidi kipanda uso ni wanawake kuliko wanaume.

"Inatakiwa kwa hali hiyo uwe na ratiba au kitabu (diary) kinachokuongoza kwamba kila kichwa kikiuma sababu ni nini? Joto, labda unakuwa unatembea na mwavuli, kofia, unajipepea au utatumia tiba ya kutuliza maumivu," alisema bingwa huyo.

Suzana Mathias, mkazi wa Kinondoni, mkoani Dar es Salaam alisema joto, hasa majira ya usiku linasababisha yeye na familia yake kukosa usingizi wenye utulivu.

"Mwanangu mdogo ana miezi 10 na kwa joto hili amekuwa anasumbua na kulia kila mara. Ametokwa na vipele vya joto, umeme ukikatika hakulaliki," alisema Suzana.

Jericko Clement, mkazi wa Dar es Salaam, alisema ongezeko la joto hivi sasa limekuwa kero kubwa nchini. "Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa (TMA) inatueleza kwamba hali hii ya joto ipo katika mikoa 10 nchini, ikiwa na kiwango cha nyuzi joto 34, ambacho ni kiwango cha juu.

"Kwa bahati mbaya, umeme nao ni changamoto, watu wanashindwa kutumia viyoyozi kupunguza adha hiyo. Maisha yamekuwa ya mateso sana na hili linaelezwa kuwa limesababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

"Tunaomba serikali itusaidie kwa kuhakikisha kwamba tunapata umeme wakati wote na pia tupate maji ya kutosha. Joto hili bila kuwa na umeme na maji ni tatizo kubwa, ambalo linaweza kusababisha matatizo mengine," alisema Jericko.

Samson Masanja, mkazi wa Kibamba, wilayani Ubungo, alisema adha ya joto inawaathiri zaidi watoto wadogo, akisema mkewe amejifungua hivi karibuni na mtoto wao mchanga ana mwezi mmoja.

"Umeme ukikatika hakulaliki. Inabidi uanze kumpepea, nje mbu na ndani joto, utatokaje kuna mbu wakali zaidi? Kumpepea na kumbembeleza hadi mtoto alale ni shughuli, utatokwa jasho sana," alilalama Masanja.

Wiki iliyopita TMA ilitaja sababu za ongezeko la joto katika baadhi ya mikoa kama vile kusogea kwa jua la utosi na upungufu wa mvua kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Ilisema katika kipindi cha Februari, mwaka huu, Mkoa wa Dar es Salaam na visiwani Zanzibar nyuzi kutakuwa na ongezeko la joto pamoja na mikoa ya Tanga ambao joto litakuwa la nyuzi joto 33, Arusha (21), Dodoma (30), Kigoma na Tabora (29), Mbeya (25), Mwanza (28) na Iringa (26).

**KABWELA** FADHILI MOHAMED





Meneja wa Tawi la BRAC wa Katesh, Lucy Mwaikena (kulia), akipeana mkono na Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janeth Mayenga, wakati wa hafla ya kukabidhi mifuko 1,413 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni 25 kwa ajili ya waathirika wa maporomoko ya matope ya Katesh. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bashe ataka sera maalum ya fedha sekta ya kilimo

**Na Maulid Mmbaga,** aliyekuwa TABORA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amesema umefika wakati wa kuwa na sera maalum ya fedha katika sekta ya kilimo, ili kuwezesha wakulima kupata mikopo yenye riba nafuu.

Amesema kwa sasa wakulima wanakopa kwenye benki ambazo zina mrengo wa kibiashara, hivyo kuna haja ya kuwa na sera ya fedha itakayohusu sekta hiyo itakayotoa fursa ya wakulima kuwa na uwezo wa kukopesheka kwa urahisi bila kuwapo vikwazo vinavyosababishwa na kutokuwapo sera maalum ya fedha kwenye kilimo.

Aliyasema hayo juzi mkoani Tabora baada ya kuzindua tawi jipya la Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ambalo litahudumia mikoa mitatu ya Tabora, Kigoma na Katavi.

Alisema kuwapo benki hiyo kutasaidia kuongeza tija kwenye sekta ya kilimo katika ukanda huo wa magharibi.

"Katika uchumi wote wa nchi yetu, mikopo inayoingia ni zaidi ya Sh. trilioni 20 na inayokwenda sekta hii ni asilimia chini ya 10.

Na bado ukienda kwenye uzalishaji katika kilimo fedha inayotolewa kama mkopo ni ndogo sana.

"Sasa nimeshaongea na Waziri wa Fedha, Gavana wa Benki Kuu, Waziri wa Mipango na Uwekezaji, ninawaandikia barua.

"Tunahitaji sera ya fedha ya kilimo kwani haiwezekani kilimo kikopeshwe kwa kutumia sera za benki za biashara, kutumia sera hiyo bado hatutoweza kutoa watu kwenye umaskini," alisema Bashe.

Aliongeza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan anafanya jitihada za kuinua sekta hiyo na kuboresha maisha ya wakulima, ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji na kupanua huduma za benki ya kilimo yenye lengo la kuleta mapinduzi ya kilimo kwa mipango endelevu inayokidhi mahitaji ya wakulima kupitia huduma tofauti za kifedha.

"Serikali ikishamaliza kuboresha miundombinu mkulima anahitaji fedha ya kununua mbolea na pembejeo. Kwa hiyo, ni muhimu na lazima tukawa na sera inayoeleweka ya kupata mitaji kwenye sekta za uzalishaji kama kilimo, mifugo na uvuvi, na mimi kama waziri nitawasukuma wote wanaohusika ili kupata sera hii na ninaamini itafanikiwa," alisisitiza Bashe.

**Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Vyama vya Ushirika Kigoma, Hussein Buchunguka, ambaye ni mkulima wa mchikichi, alishukuru benki hiyo kwa mchango mkubwa wa kuwawezesha wakulima na katika ununuzi wa mitambo ya uchakataji wa zao hilo.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya TADB, Frank Nyabundege, alisema hadi kufikia Februari, mwaka huu, TADB imewezesha wakulima na wafugaji kwa kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 19.599 katika mikoa ya Kigoma Sh. bilioni 7.209, Katavi Sh. bilioni 2.394 na Tabora Sh. bilioni 9.996.

"Mikopo hii imetolewa kwenye miradi ya mpunga, michikichi, maharage, mahindi, unenepeshaji ng'ombe, tangawizi, ufugaji kuku, nguruwe na kondoo.

"Benki inaendelea kuweka mikakati thabiti ya kukopesha kwenye zao la tumbaku, pamba na asali, kwani mazao haya yanachangia kukuza uchumi wa Mkoa wa Tabora," alisema Nyabundege.

Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Vyama vya Ushirika Kigoma, Hussein Buchunguka, ambaye ni mkulima wa mchikichi, alishukuru benki hiyo kwa mchango mkubwa wa kuwawezesha wakulima na katika ununuzi wa mitambo ya uchakataji wa zao hilo.

"Leo mchikichi unatambulika, awali ilikuwa zao la mazoea, sasa ni zao la uchumi mpaka tunavyoongea mtayaona mafuta yanayotokana na mchikichi, safari ya kuondokana na uhaba wa mafuta imeanza, asanteni kwa kutuunga mkono na kujenga heshima yetu katika kilimo," alisema Buchunguka.

# NMB yajivunia mafanikio yake Kili Marathon 2024

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

UONGOZI wa Benki ya NMB umesema unajivunia mafanikio makubwa uliyopata katika Mbio za Kimataifa za Kilimanjaro 'Kili International Marathon 2024,' zilizofanyika Jumapili zikianzia na kumalizikia kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU), mjini hapa.

Zaidi ya washiriki 10,000 kutoka mataifa mbalimbali duniani, walikimbia Kili Marathon 2024, mbio zilizohudhuriwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro. Washiriki walichuana katika kilomita 42 (full marathon), kilomita 21 (half marathon) na kilomita tano (5km fun run).

Kupitia klabu yake ya mbio za taratibu 'NMB Jogging Club,' benki hiyo 'ilitikisa' mbio hizo kupitia washiriki wake zaidi ya 150 – wakiwamo wafanyakazi wake kutoka kanda mbalimbali nchini, kivutio kikubwa kikiwa ni kikundi maalum cha vijana mabalozi wa NMB kiitwacho 'Chugga Dance' cha Arusha.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mbio hizo, Meneja Msaidizi wa NMB Jogging Club, Stella Motto, alisema benki yake imepata mafanikio makubwa katika ushiriki wao huo uliowezesha kupata allichokiita 'kuua ndege wawili kwa jiwe moja,' huku akishukuru uongozi kwa uwezeshaji.

"Tunamshukuru Mungu tumemaliza mbio salama na kimsingi tunamshukuru mwajiri wetu NMB kutupa nafasi nyingine ya kushiriki Kili Marathon kwa zaidi ya mwaka wa tano sasa, huku mwaka huu tukipata mafanikio makubwa katika malengo mawili tuliyokuja nayo.

"Tumekuja hapa ili si tu kujenga uhusiano mwema baina ya benki yetu, taasisi shiriki na waratibu, bali pia tulikuwa na malengo mawili ambayo yamefanikiwa sana, nayo ni kujenga na kuimarisha afya za wafanyakazi, lakini kunadi moja ya bidhaa zetu sokoni.

"Kupitia washiriki wetu, benki ilichagua kuitumia Kili Marathon 2024 kuinadi bidhaa yetu mpya ya NMB Pesa Akaunti, ambayo ni akaunti nafuu na rahisi zaidi nchini inayofunguliwa kwa Sh. 1,000 tu, na ambayo haina makato ya mwezi kama zilivyo akaunti zingine.

"Tumefanikiwa sana katika maeneo yote hayo, kwa sababu ushiriki wetu ulikuwa kivutio na kujenga uelewa mkubwa juu ya NMB Pesa kwa washiriki wengine, lakini kwa wananchi walioshuhudia mbio hizo kwenye barabara mbalimbali za Mji wa Moshi," alisema.

Aliongeza kuwa michezo na mazoezi ni afya na anaamini ushiriki wao unakwenda kuongeza ari ya uwajibikaji kazini na kuwapo washiriki kutoka taasisi na mikoa mbalimbali, pamoja na washiriki binafsi, kunakwenda kufikisha NMB Pesa kwa kila Mtanzania kama lilivyo lengo la bidhaa hiyo.

Meneja wa NMB Jogging Club, Shadrack Mijjinga, amejivunia ushiriki wa benki yake katika Kili Marathon, huku akipongeza maandalizi ya taasisi yake, pia ufanisi wa mbio hizo kwa ujumla wake na kuvutia washiriki mbalimbali.

"Ulikuwa msimu mwingine wa mafanikio makubwa kwetu katika mbio hizi, tulikuwa na maandalizi mazuri yaliyowezesha wengi wetu kukimbia na kumaliza vyema kwenye umbali tofauti, wengi wetu tukishiriki kilomita 21 na kilomita tano pamoja na kilomita 42.

"Tunawapongeza waratibu wa Kili Marathon kwa kufanikisha tukio hili kubwa la kimataifa ambalo halikuwa na malalamiko, wala manung'uniko kwa wakimbiaji walioshiriki mbio hizi, hata miongoni mwetu sisi NMB Jogging Club," alisema Shadrack.

Aliwataka Watanzania kuchangamkia akaunti za NMB Pesa 'Haachwi Mtuuu,' ili kuwa sehemu ya huduma jumuishi za kifedha, akaunti ambazo zinafunguliwa kidigitali kote nchini kupitia watoa huduma wa benki hiyo kinara nchini.

## Vijiji 64 kupata neema huduma majisafi, salama

**Na Dege Masoli,** KILINDI

VIJIJI 64 kati ya 102 vya Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga vimeingizwa kwenye mpango wa mwaka wa fedha 2023/2024 wa kupatiwa huduma ya maji safi na salama.

Kwa mujibu wa taarifa iliyosomwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) Wilaya ya Kilindi, Martin Malulu kwenye kikao cha robo ya pili cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kwamba vijiji 17 miradi yake inaendelea.

Katika taarifa hiyo ilieleza kuwa vijiji 24 miradi ipo hatua za mwisho za usanifu, miradi 23 inahusu ufuatiliaji wa vyanzo vya maji kwa ajili ya uchimbaji wa visima mirefu.

Hata hivyo alieleza kuwa kata mbili kati ya 21 za Wilaya ya Kilindi ndizo zinazohudumiwa na Mamlaka Ndogo ya Maji ya Mji wa Songe ambapo kata 19 zinahudumiwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira wa wilaya hiyo.

Aidha, alisema kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 Sh. 3,778 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa miradi ya maji Wilaya ya Kilindi ya kukamilisha, kuboresha na ujenzi wa miradi mbalimbali ya huduma hiyo.

Alitaja vipaumbele kuwa ni pamoja na ukamilishaji wa mradi wa

Bokwa/Mafulila, Kilindi Asilia/ Mabalanga, Diburuma/Songe, Kwamaligwa/Gitu, Bwawa la maji Msente/ MkindiMgera/ Kisangasa, Kwalugulu/ Negero, Bweawa la maji Saunyi/Lombouti, na ujenzi wa visima 23 katika vijiji.

Miradi mingine ni ujenzi wa chujio la maji Jungu/ Barang'a Lwande/Sagasa na ukarabati wa mradi wa maji

Chamtui, ununuzi wa pampu ya mradi wa maji Kwediboma pamoja na uboreshaji wa huduma ya maji Songemjini na Nkama.

Akizungumzia kuhusu changamoto, mhandisi Malulu alitaja ni ukosefu wa umeme wa uhakika na hivyo kusababisha uzalishaji wa maji kuwa chini ya mahitaji.

Changamoto nyingine ni ukosefu wa vyanzo vya maji vya uhakika na visima kuwa na asili ya chumvi ikiwamo upungufu wa watumishi na vitendea kazi.

# Dk. Mpango aiagiza VETA kuanzisha mradi ufugaji samaki

**Na Hamida Kamchalla,** MKINGA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameagiza menejimenti ya Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) kilichoko Wilaya ya Mkinga, mkoani Tanga, kuanzisha mradi wa ufugaji wa samaki ili kuzalisha wataalamu wabobezi.

Alisema ufugaji wa samaki ni zao muhimu la kiuchumi ambalo kama litapewa kipaumbele linaweza kuinua idadi kubwa ya vijana kupata ajira.

Alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na menejimenti ya chuo hicho.

"Muhakikishe kwamba chuo hiki kinawezeshwa uanzishwaji wa ufugaji wa samaki mara moja, ndugu zangu maelekezo ninayoyatoa ningeomba sana myazingatie na kuyatekeleza" alisema. Aidha aliwataka wananchi wilayani hapa kujitahidi kupanda miti katika kaya zao na kuweka hali nzuri ya utunzaji wa mazingira ili kuepuka majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi yanayotokea.

Alibainisha kwamba ni muhimu pia kuhakikisha mazingira ya chuo hicho yanakuwa bora ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na utaratibu wa kujifunza kulinda na kutunza mazingira.

"Kwa hiyo niwaombe wananchi, taasisi binafsi, taasisi za kidini na wadau wengine kushirikiana na serikali kutengeneza wataalamu wengi zaidi kwenye fani mbalimbali, lakini hasa katika masomo ya sayansi, ubunifu, teknolojia na ufundi," alisisitiza.

Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Tanga, Mwanaisha Ulenge, alisema uwepo wa chuo hicho wilayani hapa utasaidia vijana kujikwamua kiuchumi na maendeleo kuweza kupatikana.

Ulenge aliiomba serikali kuweza kufanya ukarabati wa jengo la maktaba ya Mkoa wa Tanga kutokana na uchakavu uliopo kutokana na kujengwa miaka mingi.



Mratibu wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Julius Mgeni (kulia), akizungumza na wajumbe katika kikao cha mpango wa umezaji wa dawa tiba na kinga dhidi ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele juzi, mgeni rasmi alikuwa Ofisa Tarafa ya Muheza, Japhet Hayule, shughuli ya umezaji dawa itaanza Februari 28-29 mwaka huu na walengwa ni watu 200,258 wa wilaya hiyo ambao watameza dawa ya usubi, minyoo na kichocho. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Ummy: Maambukizi VVU Tanga yapungua

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) katika Mkoa wa Tanga yamepungua kutoka asilimia 4.4 hadi asilimia 2.9.

Alitoa takwimu hizo wakati akikabidhiwa vifaa vya kuboresha huduma za afya katika kupambana na magonjwa ya VVU na kifua kikuu katika Hospitali ya Rufani Bombo.

Vifaa hivyo ni pamoja na pikipiki 50, majokofu 72, sentimita 56, kompyuta 50, UPS 50 na printa 50 ambavyo vimegharimu Sh. milioni 800.

Vifaa hivyo vimetolewa na Shirika la Tanzania Health Promotion Support (THPS) kwa ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia kituo chake cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa (CDC).

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Ummy alimtaka Mganga Mkuu wa hospitali hiyo, Japhet Simeo, kushirikiana na watumishi wengine kuhakikisha wanaendelea kuhamasisha wananchi wa rika zote kupima VVU pamoja na kuwapa elimu.

Aidha, alitoa maelekezo na kusema kuwa Wizara ya Afya imejipanga kufikia asilimia 95 ya wagonjwa wanaojitambua hali zao kuwa na maambukizi kitaifa ifikapo mwaka 2025 ambapo alibainisha kwamba mpaka sasa Mkoa wa Tanga umejitahidi katika makundi mawili kufikia malengo hayo.

Kuhusu wajawazito alisema: "Tunataka kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, kitaifa tupo asilimia 6.9, hivyo tunataka tufikie angalau chini ya asilimia nne mwaka 2025".

Pia alitaka kufikiwa kwa wanaotumia dawa za kulevya na kujidunga sindano ili kuweza kupunguza maambukizi, ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi.

Vilevile aliwaomba wafadhili wanaounga mkono juhudi za serikali kuwafikia wagonjwa wa kifua kikuu kwa kushirikiana pamoja na jamii, viongozi wa dini na kimila lakini pia waganga wa jadi kutokana na utamaduni kwamba wananchi walio wengi hupenda kukimbilia huko.

# Misaada waathirika Hanang' yazidi kumiminika

**Na John Badi**

MISAADA mbalimbali imezidi kumiminika kwa waathirika wa mafuriko wilayani Hanang' mkoani Manyara, safari hii mifuko ya saruji yenye thamani ya Sh.milioni 25.

Msaada huo umetolewa juzi na kampuni ya Brac Tanzania Finance Ltd (BTFL) inayojihusisha na masuala ya kifedha.


Mafuriko hayo yaliyotokea Desemba mwaka jana mjini Katesh kusababisha familia nyingi kukosa makazi na kukabiliwa na changamoto kubwa katika ujenzi wa nyumba zao na jamii.

Meneja wa Mawasiliano BTFL, Emma Mbaga, alisema wanalenga kuchangia juhudi za ujenzi na kusaidia kupunguza baadhi ya mizigo inayowakabili waathirika wa mafuriko.

Alisema saruji ni nyenzo muhimu ya ujenzi ambayo itakuwa muhimu katika kujenga nyumba, miundombinu na vifaa vya jamii ambavyo vimeharibiwa na mafuriko.

"Katika nyakati za shida, ni muhimu kwa mashirika na jamii kuja pamoja kushirikiana na kutoa msaada kwa wale wanaohitaji. Tulihuzunishwa sana na maafa na uharibifu uliosababishwa na mafuriko na matope huko Katesh ambayo yameathiri wananchi wenzetu wengi," alisema.

Makabidhiano ya mifuko 1,413 ya saruji yalifanyika katika ofisi ya Wilaya ya Hanang' mjini Katesh na mchango huo ulipokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Kateshi, Janeth Mayenga.



# Mwenyekiti Kitongoji mbaroni tuhuma kumjeruhi mhudumu

**Na Timothy Itembe,** TARIME

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Majengo Mapya wilayani Tarime, Silas Nyamhanga (46), anashikiliwa na Jeshi la Polisi Kanda Maalum Tarime-Rorya kwa tuhuma za kumpiga na kumjeruhi mhudumu wa baa, Jenipher Shaban (31).

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Marck Njera alisema chanzo cha kijana huyo kumjeruhi dada huyo ni baada ya kumdai Sh.24,000 alizokunywa pombe.

Akithibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo Kamanda Njera alisema baada ya kupata taarifa ya tukio hilo lililoripotiwa Februari, 17 mwaka huu, walianza uchunguzi na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa huyo.

Kamanda Njera alisema mtuhumiwa anakabiliwa na tuhuma za kumjeruhi kwa kushambuliwa kwa rungu, ngumi na mateke sehemu mbalimbali za mwili na kung'oka meno mawili.

Alisema chanzo cha tukio ni mtuhumiwa kudaiwa Sh.24,000 alizokunywa pombe katika baa hiyo, ambapo mtuhumiwa alimhadhaa mwanamke huyo na kumpeleka nyumbani kwake ili akamlipe, badala yake alimfungia ndani ya uzio na kuanza kumshambulia.

"Kwenye nyumba hiyo alikuwapo mke wa mtuhumiwa na kijana wake wa kiume ambaye ndiye aliyefungua mlango wa geti na mwanamke huyo kupata nafasi ya kujinusuru katika shambulio hilo," alisema Kamanda Njera.

Alisema mlalamikaji alipatiwa PF.3 kwa ajili ya matibabu na hali yake inaendelea vizuri baada ya taarifa hiyo kupokelewa na Jeshi la Polisi lilichukua hatua ya haraka kumsaka mtuhumiwa na kumkamata.

Kamanda Njera alisema upelelezi wa shauri umekamilika, jalada limepelekwa kwa Wakili wa Serikali kwa ajili ya kuandaa mashtaka ili aweze kufikishwa mahakamani.



Wachuuzi wa mahindi wakichagua bidhaa hiyo katika soko la Mawasiliano jijini Dar es Salaam jana, yaliuzwa kwa Sh. 300. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wakulima watahadharishwa matumizi ya mbegu bandia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKULIMA nchini wametakiwa kuwa makini wanapokwenda kununua mbegu, kuepuka ununuaji wa mbegu bandia zisizoweza kuwapatia mavuno stahiki.

Bali wametakiwa kutafuta mbegu zilizothibitishwa na taasisi husika zitakazowasaidia kupata mavuno mengi na kuwainua kiuchumi.

Wito huo umetolewa juzi na Ofisa Mthibiti Ubora wa Mbegu kutoka Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), kutoka makao makuu Morogoro, Zera Mwankemwa.

Alisema matumizi ya mbegu za kilimo zisizo na ubora husababisha wakulima kutopata mavuno mengi na hata kushuka kiuchumi, lakini wakitumia mbegu zilizothibitishwa na TOSCI watapata mavuno mengi na kuinuka kiuchumi wao na taifa kwa ujumla.

"Mfano mkulima akinunua mbegu za mahindi kilo mbili zenye ubora zilizothibitishwa kwa hekali moja atatumia mifuko minne, na akija kuvuna mazao yake atapata magunia 13 ya mahindi hadi 15, tofauti akitumia mbegu zisizo na ubora atapa magunia mawili au matatu," alisema Mwankemwa.

Ofisa Mkaguzi kutoka TOSCI, Joseph Pagu, alisema ili kubaini mbegu zilizothibitishwa na kuepuka kununua mbegu bandia, mkulima atatakiwa kukwangua kama vocha eneo lenye lebo ya TOSCI, kisha ataona namba watakayoingiza kwenye simu na kupata majibu kama imethibitishwa kweli.

"Wakulima watabonyeza *148*52* wataingiza namba ambapo zipo kwenye lebo ya TOSCI, baada ya kuzikwangua kama vocha, kisha wanaweka alama ya reli na kupiga watapata majibu hapo hapo mbegu hizo ni bora," alisema Pagu.

Hivyo, aliwasisitiza wakulima kwamba kila msimu wa kilimo unapofika ni vyema wakawa wananunua mbegu na siyo kutumia mbegu ambazo zimesalia kwenye mavuno na kuzipanda tena.

Alisema endapo watatumia mbegu ambazo zimesalia kuna uwezekano mkubwa kutopata mavuno mengi.

# Wajasiriamali Stendi ya Nyegezi walia kunyanyaswa, kupigwa

**Na Remmy Moka,** SAUT

WAJASIRIAMALI wanaofanya biashara katika Stendi Kuu ya Mabasi Nyegezi iliyopo jijini Mwanza, wameulalamikia uongozi wa kituo hicho kutumia mabavu na kuwanyanyasa wanapokuwa katika shughuli zao.

Walitoa malalamiko hayo juzi wakati Mwenyekiti wa CCM Kata ya Nyegezi, Enock Nyabange pamoja na Mtendaji wa Kata hiyo, Shabani Msuya walipofika katika kituo hicho kusikiliza na kutatua kero za wafanyabiashara hao.

Wakitoa malalamiko hayo, Hassan Nasoro alisema miongoni mwa manyanyaso wanayokabiliana nayo ni pamoja na kuzuiwa kuingia katika kituo hicho kufanya biashara zao, licha ya kuwa tayari wamelipia vitambulisho zaidi ya 1,000 ambavyo bado havijatolewa na uongozi huo.

"Pia mgambo wa hapa wamekuwa wakitumia nguvu jambo linalosababisha migogoro mikubwa baina ya sisi, migambo na uongozi wa stendi," alisema Nasoro.

Mfanyabiashara mwingine, Thomas Njao alisema licha ya wafanyabiashara hao kupunguziwa ushuru kutoka Sh. 8,000 hadi Sh. 2,000 bado wamekuwa wakiangaika na maeneo ya kufanyia shughuli za kibiashara hasa mamalishe ambao hawaruhusiwi kuuza chakula ndani ya stendi hiyo.

Pia alilalamikia uwapo wa huduma mbovu ya choo ambapo wamekuwa wakitozwa ushuru licha ya wao kuchangia mapato ya ushuru wa stendi.

Hivyo, aliiomba serikali kuwatambua mchango wao na kuwapunguzia mzigo mkubwa wa tozo.

Mtendaji wa Kata hiyo, Shambani Mpuya aliwataka wafanyabiashara hao kuwa na utaratibu wa kuwasilisha kero zao katika maeneo husika, ili kupunguza maumivu wanayokaa nayo bila kutatuliwa. Alimtaka Meneja wa Stendi kuhakikisha anasimamia sheria ipasavyo.

Akijibu kero hizo, Meneja wa Stendi hiyo, Francis Ngassa alisema wafanyabiashara hao wamekuwa hawaongei yanayowasibu.

Alisema baadhi ya kero alizisikia kwenye mkutano huo na kuwataka kuchagua viongozi makini watakaowasaidia kufikisha mahitaji yao sehemu husika kwa wakati.

Hivyo aliahidi kufanyia kazi baadhi ya kero ambazo zipo ndani ya uwezo wake na kuwataka wafanyabiashara hao kuendelea kuwa watulivu wakati akiendelea kushughulikia matatizo hayo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Nyegezi, Enock Nyabange aliwataka watendaji wanaofanya kazi ndani ya stendi hiyo kushirikiana na kuondoa tofauti zao baina ya wajasiriamali na viongozi wa stendi, kwani baadhi ya changamoto zinatokana na kutokuwa na ushirikiano baina yao.

Pia aliutaka uongozi wa eneo hilo kuweka utaratibu wa kutoa elimu ya kutosha kwa wajasiriamali ili kuondoa kero na vilio, kwamba baadhi ya matatizo yanasababishwa na ukosefu wa elimu kwa wajasiriamali pamoja na uwajibikaji wa viongozi husika.

Nipashe

# TESA

Jumanne Februari 27, 2024

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

Mapinduzi teknolojia janga jipya kwa watoto



Ukurasa 13

Maji ni kilio kila kona, utoro darasani, watu, mifugo, wanyamapori wala sahani 1



Ukurasa 14

**Mteja wa maji, umeme tambua haki, wajibu na wakumfikishia kero zako**

ELIMU

NA BEATRICE SHAYO, ALIYEKUWA KIGOMA

## SIMULIZI YA MTOTO ALHAJI

# Ilivyoitoa familia gizani kuiingiza katika nuru

DAKIKA tatu za Alhaji Hussein (10), mbele hadhara na viongozi wa chama na serikali, zimetosha kubadili maisha yake na jukumu la kuilea familia badala ya kusoma na sasa yuko darasani.

Alhaji aliacha shule akiwa darasa la tatu akiwa Shule ya Msingi Kabingo iliyoko Kigoma na kuanza kuuza ndizi mbivu akizizungusha mitaani ili kupata fedha za kujikimu pamoja na mama na ndugu zake watano.

Ni mtoto wa pili kuzaliwa katika familia yao inayoishi Gungu Masanga Manispaa ya Kigoma Ujiji ambaye ameandika historia baada ya kutoa ya moyoni na sasa maisha yamebadilika, yuko darasani akijiandaa na mtihani wa darasa la nne.

Mtoto huyo ni mcheshi anayejua kuyapangilia maneno ikilinganishwa na umri wake, inabainika anapoeleza hali ya maisha yake kwa Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzi wa CCM, Paul Makonda.

Anasema wanaishi kwenye chumba kimoja na kulala chini kwenye mikeka, akitoa maelezo hayo mwanzoni mwa mwezi huu kwenye viwanja vya Mwanga Center Kigoma.

Akiwa na beseni la ndizi, anaomba kipaza sauti kwa ajili ya kuomba kusaidiwa ili arudi tena shuleni.

Anaeleza kuwa biashara anayoifanya si kwa mapenzi yake ni kutokana na ugumu wa maisha aliyonayo ili kuitunza familia yake.



Alhaji (kulia) akifurahi na wenzake baada ya kurejea darasani. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

Baada ya kumsikiliza mtoto huyo Makonda anamuuliza anahitaji kusaidiwa nini? Anamjibu kurudi shuleni, kupatiwa kodi ya nyumba ili asiendelee kuuza ndizi na mama yake apate mtaji wa biashara, ili aanzishe biashara.

Anaeleza kuwa afya ya mama inaimarika baada ya kuumwa kwa muda na atakapopata mtaji atafanyabiashara na kuwapatia chakula naye atarudi darasani.

Makonda anaguswa na ombi hilo anatoa Sh. 1,000,000 na kuanza kuchangisha viongozi, lakini pia wananchi waliguswa wakachanga zikapatikana Sh. milioni 2.22 anazoagiza apelekewe mama Alhaji ziwasaidie na kuahidi kumsomesha mtoto huyo.

Taarifa za mtoto huyo zilisambaa na kumfikia Rais Samia Suluhu Hassan, anayeahidi kumsomesha Alhaji na sasa yuko darasani, pamoja na wadogo zake, kuwajengea nyumba, kuweka samani na kumwezesha mama yake kwa mtaji wa Sh.5,000,000 na kuwapatia bima ya afya.

Nipashe inazungumza na Alhaji nyumbani kwao Gungu Masanga, akieleza kuwa kwa miaka miwili amefanya biashara ya kutembeza ndizi mbivu maeneo ya Kigoma mjini, SIDO na Mwanga.

Anakumbusha kuwa mwaka 2022 alilala na njaa baada ya kurudi nyumbani akitoka shule kwa vile hakukuwa na chakula na mama alikuwa mgonjwa.

Anaeleza kuwa kukosekana chakula nyumbani kulimuumiza, akapeleka kilio chake kwa mwanajeshi mmoja aliyempatia Sh. 4,000, alizotumia kuanzisha biashara hiyo.

"Nilikaa hata siku mbili bila chakula. Ni Mungu alimtumia mwanajeshi kuongea nami tulikutana stendi mpya ya mabasi Kigoma nikamwambia sijala akaninunulia juisi akanipa Sh.4,000 akaniambia tukale chakula," anaeleza Alhaji.

Anasema baada ya kupata fedha hiyo wazo la kufanya biashara likamjia lakini ipi? Hata njaa aliyokuwa nayo aliisha, akitosheka na juisi, aliyopewa akaondoka hadi soko la Nazareti lililopo Kigoma Mjini kununua ndizi.

"Niliacha shule. Maisha yalikuwa ni magumu sio kwamba nafurahia kufanya biashara ya ndizi hapana...ninapitia magumu tunakosa chakula. Mama yangu alikuwa anaumwa ilinilazimu nihangaike kumsaidia na wadogo zangu wapate chakula," anasema Alhaji.

Mbali na kutafuta fedha ya chakula anasema kuna wakati alilipa Shilingi 20,000 kodi ya nyumba kwa mwezi.

"Mtaji wangu wa ndizi uliongezeka hadi kufika Sh. 20,000 kodi ilikuwa imekwisha ikabidi nitoe fedha hizo kwa mama akalipe maana mwenye nyumba alianza kumsumbua, siku hiyo hatukuwa na chukula," anaeleza Alhaji.

Baada ya kulipa kodi hakuwa na akiba yoyote, alikopa ndizi kwa wateja wake ili aendelee na biashara, alifanikiwa na kwamba anapata faida Sh. 2,000 hadi Sh. 5,000 kwa siku na kumwezesha kununua chakula walau wasikose mlo mmoja.

"Ikifika jioni nilikuwa narudi nyumbani na mboga nachukua dagaa na unga mara nyingi chakula chetu ni cha jioni. Fedha inayobaki nampatia mama kununua dawa na nyingine akiba na kodi ya nyumba," anasema na kuongeza kuwa ananunua ndizi nne kwa Sh 500 hadi Sh. 700, anazoziuza Sh.200 kila moja.

**YALIYOMKUTA**

Kudhihakiwa kwa kuambiwa unatakiwa kuwa shuleni na si kufanyabiashara ni miongoni mwa mambo aliyokutana nayo

"Yupo aliyeniambia nikikuona unakanyaga huku mjini nitakukamata... naogopa kupita na beseni langu huko mjini ni vile hajui mapito yangu na pambana mama yangu na wadogo zangu wasilale na njaa."

Anasimulia kuwa kuna wakati wakiwa chumbani na

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA MAULID MMBAGA

# Mapinduzi teknolojia janga jipya kwa watoto

## • Ni vifo, mtoto huingizwa mtandaoni kila sekunde

ONGEZEKO la kasi ya matumizi ya intaneti Afrika na pia Tanzania takribani miongo miwili iliyopita yamefungua mengi, kuanzia kukuza uchumi hadi kuongeza uelewa na mbinu za kukuza ufahamu na ujuzi.

Lakini, mapinduzi ya kidijitali hayajawaacha wengi salama. Ni athari na majanga kila kona na hata watoto ni waathirika wa matumizi mabaya ya intaneti.

Kutumia vifaa vya kielektroniki kuanzia kompyuta, simu na televisheni kumechochea ukatili wa kimtandao kwa watoto na kuwasababishia madhara ya kudumu.

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), watoto wanatumia muda mwingi mtandaoni kuliko awali, na kwamba duniani kote, mtoto huingia mtandaoni kwa mara ya kwanza kila baada ya nusu sekunde.

UNICEF inasema unyanyasaji wa mtandaoni unaweza kuathiri watoto kila wakati wanapoingia kwenye mitandao ya kijamii au majukwaa ya ujumbe wa papo hapo, na kwamba wakati wa kuvinjari wanaweza kukabiliwa na ujumbe wa chuki na maudhui hatari mengine yakichochea kujidhuru na hata kujiua.

"Watoto wanaweza kuumizwa kupitia kutayarisha, kusambaza na kutumia nyenzo za unyanyasaji wa kijinsia, au wanaweza kutayarishwa kwa ajili ya kunyanyaswa kingono, huku wahusika wakijaribu kukutana nao ana kwa ana au kuwahimiza watoe maudhui machafu," inasema UNICEF.

Thelma Dhaje ni Mkurugenzi wa Taasisi ya CISEMA ya Dar es Salaam, inayojihusisha na kutetea haki za watoto, akizungumza na Nipashe, anasema tatizo la kimtandao kwa watoto linaongezeka kwa kuwa kila kunapowekwa vizuizi vya unyanyasaji watu wanabuni mbinu mbadala kufanya kile wanachodhamiria kwa watoto.

"Huwezi kutofautisha ukatili unaofanyika mtandaoni na ule wa mazingira ya kawaida, inawezekana mtoto akafanyiwa ukatili au kubakwa na akarekodiwa katika mazingira ya kawaida na ukahamishiwa katika mtandao jambo litakaloathiri maisha yake yote," amesema Dhaje.



Watoto na teknolojia ya simu. **PICHA: MTANDAO**

### KATUNI NI SHIDA

Mkurugenzi wa CISEMA, anaeleza kuwa dunia inatambua kuwa watoto wengi hupenda kuangalia katuni kwenye televisheni, simu au kompyuta hivyo wasiokuwa na nia njema hutumia nafasi hiyo kutengeneza programu zenye kutambua wakati na mahali mtoto anapoangalia katuni kupitia vifaa vya intaneti.

Anafafanua kwamba watu wanaoendesha programu hizo baada ya kutambua kuwa kuna mahali mtoto anatazama katuni kwa kutumia simu au kompyuta huzidukua na kuziweka katika mfumo unaowawezesha kuwasiliana nao moja kwa moja na kumrubuni kwa maneno na baadaye kumwamrisha kufanya vitu ambavyo ni kinyume na maadili.

"Baadhi ya programu hizo za katuni zimetengenezewa mtu mwenye sura ya kitoto ambaye anatumika kuongea na mtoto anayetazama na kumfanya aamini kuwa anaongea na mtoto mwenzake, baadaye humshawishi avue nguo na kuonyesha maungo huku akijirekodi.

"Katuni zimeonekana ni chanzo cha mtoto kufanyiwa matendo maovu na nyingine humwandaa kufanya mambo ambayo ni kinyume na maadili 'online gruming child for sexual pupose'."

Anatoa rai kwa watoto, wazazi au walezi kuwa makini na kuepuka kuwaachia watoto kuangalia vitu hivyo kwenye simu au kompyuta wakiwa wenyewe.

Ananukuu utafiti uliofanywa mwaka 2022 kwa watoto wenye umri wa miaka 12 hadi 17 umebainisha kwamba asilimia 67 ya watoto wanatumia mitandao ya kijamii kama facebook, X (twitter), instagram, whatsap, tiktok na telegram.

Aidha, inabainisha kuwa asilimia nne ya watoto waliotumia mitandao hiyo walifanyiwa aina tofauti za ukatili, pamoja na kukutana na wahalifu waliowasiliana nao moja kwa moja kupitia mtandao. Huku asilimia tano wakikutana na vitisho, kushawishiwa na kulazimishwa kutuma picha zao za utupu.

Mhadhiri wa elimu na saikolojia, katika Chuo Kikuu cha Ualimu Dar es Salaam (UDSM) Dk. Hezron Onditi, anaunga mkono hatari ya simu akisema kuwa watoto wengi wameathirika kutokana na matumizi ya simu.

Onditi mtafiti wa masuala ya teknolojia na vyombo vya habari katika ukuzaji wa watoto na vijana, anashauri jamii ibadilike na kuwalinda watoto.

Anadai kwamba kuna wazazi wanawapa watoto uhuru wa kuchezea simu kupitiliza bila kujua kuwa wanawaharibu huku wengine wakifikia kiwango cha kuvitambua vifaa hivyo kuliko wazazi jambo ambalo linageuka kuwa gumu kuwadhibiti katika matumizi.

"Kutumia teknolojia ni haki yao hatuwezi kuwazuia ila kitu tunachotakiwa kufanya ni kuhakikisha kwamba vifaa tunavyowapa wanavitumia kwa usahihi katika kusoma na kujiongezea uelewa na sio kutazama vitu vinavyowaharibu kimaadili," anashauri Onditi.

### HATUA ZA SERIKALI

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalumu, Dk.Dorothy Gwajima, anasema serikali inakusudia kuweka mkakati madhubuti kama kupitia sheria na kanuni kudhibiti ukatili wa watoto mtandaoni.

Anasema teknolojia inakwenda kwa kasi na maudhui yanayosambaa mtandaoni ni hatari kwa watoto hivyo elimu haina budi kutolewa kwa walezi na wazazi kwakuwa wamejisahau na kuwapa watoto hao vifaa vya kielektroniki ikiwamo simu pasipo kuwa karibu nao kujua nini wanakitazama.

"Tunakwenda kutoa mwarobaini, kumekuwapo na jitihada mbalimbali za kisera na kisheria za kimataifa, kikanda na kitaifa katika kuwalinda watoto na vijana balehe dhidi ya ukatili wa mitandaoni zikiwamo sheria ya makosa ya kujamiiana ya 1998.

# Ilivyoitoa familia gizani kuiingiza katika nuru

INATOKA UK.11

wadogo zake wanalia na kunyamaza wanapokosa chakula jambo lililokuwa linamuuliza.

Changamoto nyingine aliyokuwa anapitia ni kukutana na wanafunzi wenzake ambao wako darasa la tano, yeye akiendelea na biashara, wakimwambia arudi shuleni na pia wakimpa pole.

"Tatizo jingine nimekueleza kuna wakati nilikopa ndizi baada ya mtaji wangu kulipa kodi walikuwa ni wakali nisipopeleka fedha walinitishia hadi kuninyang'anya beseni, nilipambana nikalipa,"anaongeza.

### MAISHA YAMEBADILIKA

Tangu alipotoa kilio chake kwa Makonda na kupatiwa fedha na pia Rais Samia kuahidi msaada maisha yao yamebadilika wanakula, kushiba na sasa yeye na wadogo zake wanafurahia elimu yao.

"Mungu ni mwema tangu ile siku niliyozungumza pale jukwaani tunakula na kushiba Mungu amesikilia kilio chetu kuja kwenu imekuwa faraja kwetu. Mungu ambariki Rais Samia na Makonda," anasali. Ester Hussein ni mama wa Alhaji, anayesema ana watoto watano na mumewe alimtelekeza akimwacha na mapacha wa mwaka mmoja, akiaga anakwenda kumsalimia mama yake mgonjwa.

Mpaka sasa ni miaka saba imepita na alipoanza kuumwa mwaka 2021 alijulishwa, ila hakutaka kuja wala kuwasalimia watoto wake, anasema Ester.

Anaeleza kuwa kitendo cha Alhaji kufanya biashara na kuacha shule kilimuumiza lakini hakuweza kumzuia kwa kuwa alikuwa anaumwa tena hakukuwa na msaada kwa familia yake.

Anasema baada ya kupata nafuu alianza kufanya vibarua vya kulima kwa siku akilipwa Sh. 3,000 kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 10 jioni.

"Kuna siku naamka vibaya lakini pamoja na watoto wangu tunalima tukilipwa hiyo 3,000 tunapata ya kula ugali na mboga. Kuna muda hatupati chakula hayo maisha tumeyazoea," anasema.

Anashukuru ujasiri wa mtoto wake kuzungumza magumu wanayoyapitia na hatimaye kupatiwa msaada.

Shakila Issa ni jirani yao anasema familia hiyo inaishi katika mazingira magumu lakini kuwasaidia kwa kuwa naye hana kipato.

"Kupata chakula ni shida sisi majirani tuliumia kuona Alhaji anajitishwa beseni la ndizi kuzunguka mitaani ili wapate hela ya kula...," anasema Shakila.

Diwani wa Kata ya Gungu, Bakari Kathberti, anasema atasimamia maelekezo ya serikali ya kumsaidia Alhaji kurudi shuleni mama yake kuanza biashara.

### MWALIMU AMSIFIA

Msaidizi Said Shaaban, Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Kabingo, anaposoma Alhaji, anamsifu kwa mahudhurio na bidii ya kujifunza.

Shaban anasema awali alikuwa na changamoto mbalimbali zilizomkwamisha kufanya mitihani na kuacha shule, lakini wakati huu amedhamiria kusoma kwa bidii.

ELIMU

NA JUMBE ISMAILY, IKUNGI

# Maji ni janga kila kona, utoro darasani, watu, mifugo, wanyamapori wala sahani 1



Miundombinu iliyojengwa kusambaza maji maeneo mbalimbali vijijini. **PICHA:JUMBE ISMAIL.**

VILIO vya joto, jua kali, kiu na vipele vya joto vinasikika karibu Tanzania nzima, kila mmoja wakati akihitaji maji ya kunywa na ya kuogo kupoza mwili.

Lakini, kwenye vijiji vingi vilivyoko kata ya Mwaru mkoani Singida kuanzia Mpuguzi, Mlandala, Kaugeri na Mduguyu ni kila mtu kupambana na hali yake.

Wananchi wanaozungumza na Nipashe wanalia kuwa hakuna maji. Inabidi kuyasaka kwa kutembea kilometa nyingi tena kwa kuungua jua, kutoka jasho jingi, wakiwa na kiu, wakipita mbugani na vichakani ambako wanyama hatari, nyoka na wadudu wawatishia maisha.

Wanasema kauli mbiu ya kumtua ndoo mama kichwani haitekelezeki na hivyo kinamama na mabinti hutembea kilomita hadi 37 kufuata maji iwe ni mchana kutwa au usiku kucha.

Wananchi wanaeleza kuwa wanaotumia mikokoteni au tela za kukokotwa na wanyama wakiondoka saa 10 jioni hurejea usiku wa manane au alfajiri.

Aidha, haijawezekana kumtua mama ndoo kichwani katika kata na vijiji hivyo kuanzia Kijiji cha Kaugeri hadi cha Mpugizi, ambacho hakijawahi kupatiwa majisafi tangu Uhuru wa Tanzania miaka 63 iliyopita.

Licha ya vilio kufikishwa Wizara ya Maji mambo yanazidi kuwa magumu kwa kaya 872 za Mpugizi, ambazo idadi kubwa ya wananchi ni wakulima, wafugaji na wfanyabiashara wadogo.

Changamoto za kukosa maji kwa kinamama hao ni nyingi, wanapozungumza na Nipashe wanataja ugomvi kwenye ndoa zao, kuumizwa na wanyama wakali, mabinti na watoto kushindwa kwenda shuleni, utoro shuleni, kuacha kuzalisha na kuhangaika na maji, maradhi hasa ya ngozi, mazingira kujaa vumbi na kwa ujumla kuongezeka umaskini.

Wanasema kukosekana huduma hiyo kunawalazimisha wana kata ya Mwaru mfano Kaugeri kunywa na kutumia maji machafu ambayo pia huchangia na wanyama kama fisi, mbwa, ndege na mifugo yao.

Tatu Kiula anasema kwa miaka mitatu sasa amekuwa akitumia maji machafu yaliyotuama yenye utando wa kijani na taka taka nyingi kupikia, kunywa, kuogea na kufualia akiamini maisha ya wananchi kijijini hapo yanalindwa na Mungu.

"Tunalindwa na Mungu tupo hatarini tunaishi na magonjwa ya kuhara, kichocho, malaria, kipindupindu, vipele kwenye ngozi."

Anaikumbusha serikali kutekeleza kauli mbiu ya Wizara ya Maji ya kumtua mama ndoo kichani badala ya kubakia kwenye makaratasi huku watoto wakishindwa kusoma.

Aidha, anasema kuna mashine ya kuchimba visima ilifikishwa kijijini hapo lakini ilidaiwa ilivunjwa na mwamba ardhini na hakuna maji zaidi ya wanayopata kwenye madimbwi, malambo na makorongoni.

Samweli Tano, ni mkazi wa Kaugeria analalamikia wananchi kulipishwa gharama kubwa na wafanyabiashara waliochimba malambo kunywesha mifugo.

Tano anasema kijijini hapo kuna lambo la mtu binafsi na wanapotaka maji wanalipa Shilingi 300 kwa ndoo ya lita 20 ili kutumia na kunywesha mifugo yao.

Hata hivyo jamaa wa mmiliki wa malambo ambayo baada ya kuyachimba mvua ndiyo inayoyajaza maji, wanajitetea kuwa mradi huo ulianzishwa kusaidia wanakijiji ambao walifuata maji Kijiji cha Mlandala kilochoko kilometa 28 kwenda na kurudi.

Wanasema mwananchi wanapotoka saa 10 jioni wakitumia tela wanaweza kurudi saa 8:00 za usiku na kwa anayetumia baiskeli hutumia saa tatu kufika Mlandala hivyo saa sita kwenda na kurudi kijijini hapo kunakopatikana maji ambayo hata hivyo siyo safi kwa kunywa.

Aidha, wamiliki hao huwatoza Shilingi 50,000 kwa mwezi wafugaji wanaopeleka mifugo lamboni na kwa wastani hukusanya Shilingi 45,000 mpaka 50,000 kwa siku fedha wanazosema wanazitumiwa pia kuendeleza kuchimba malambo mengine.

Wawekezaji hao wenye lambo tangu kuanzisha mradi huo miaka sita iliyopita wamejikusanyia Shilingi 810,000,000, kwa mujibu wa maelezo yao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kaugeri, Jonathan Ofungwa, anaeleza kuwa upatikanaji maji kijijini humo ni ndoto na kwamba wanatumia maji pamoja na wanyama wafugwao na wa porini na ndege.

**RUWASA IMEWATOSA**

"Baada ya wananchi kupaza sauti kwa waandishi wa habari watumishi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) wilayani Ikungi, Julai mwaka jana walifika kijijini hapa na kufunga bomba wakiahidi kurudi ili kusambaza lakini mpaka sasa hawajarudi." Anasema Ofungwa.

Aidha, mwenyekiti wa kijiji hicho chenye kaya 872 za wakazi wanaoishi kwa kuhofia usalama wa afya zao kutokana na kunywa maji mchafu, anasema shirika la kimataifa la Canada limewachimbia kisima.

Ofungwa anasema ni kisima kifupi ambacho kinategemewa na wananchi lakini hata hivyo hakitoshelezi mahitaji ya wanakijiji.

Anawataka viongozi wilayani Ikungi kuwasukuma RUWASA kurudi tena Kaugeri kusambaza maji ili kuwatua ndoo kichwani wananchi hasa kinamama wanaosotea maji muda mwingi wa maisha yao.

Diwani wa Kata ya Mwaru kilipo kijiji hicho, Iddi Makangale anasema hali ya maji katika kata hiyo ni mbaya kupindukia.

Anafafanua kwamba kati ya vijiji vitano vilivyopo katika kata hiyo vya Mwaru, Mpuguzi, Mlandala, Kaugeri na Mduguyu ni Mlandala pekee kunakopatikana maji.

Makangale anasikitika akisema kuwa Kijiji cha Mpugizi hakijawahi kupatiwa maji tangu uhuru hali inayowafanya waendelee kunywa maji ya madimbwi na malambo na kushirikiana na wanyama porini na wafugwao na mbaya zaidi baadhi ya watu huoga kwenye madimbwi hayo bila kujali kuwa wenzao wanakunywa na kupikia.

Makangale, anazungumzia kisima kilichochimbwa na wahisani kutoka Canada kinachotumia nishati jua au sola kilichopo kijiji cha Kaugeri, akisema licha ya kutoa maji hakitoshelezi mahitaji ya wananchi.

Anaongeza kuwa wapo wanaoendelea kutumia maji ya madimbwi yanayochafuliwa na wanyama pori na wafugwa.

Kwa mujibu wa diwani huyo ni asilimia mbili tu ya wananchi wa kata ya Mwaru wanaopata majisafi na salama wakati asilimia 98 wanategemea madimbwi na malambo.

**KIMYA WIZARANI**

Makangale anabainisha pia kwamba alishawahi kwenda kufikisha kilio hicho ofisini kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji Dodoma.

"Baada ya kusikilizwa Meneja wa RUWASA Wilaya ya Ikungi alitakiwa kuandika andiko linaloonyesha kuwa kisima kilichochimbwa Kijiji cha Kaugeri kina maji ila kinahitaji fedha za kununulia miundombinu jambo ambalo mpaka sasa halijulikani kuwa limefikia wapi."

**WANASUBIRI BAJETI**

Akizungumzia hali ya upatikanaji wa maji katika Kijiji cha Kaugeri, Meneja wa Wakala wa RUWASA wilayani Ikungi, Hoppeness Liundi, anasema kwa sasa hakuna mradi wowote wa maji na kuahidi kwamba katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2024/2025 Kijiji cha Kaugeri kilingizwa kwenye miradi ya maji ya kuchimba visima.

ELIMU

NA LATIFA MZUNGU

# Mteja wa maji, umeme tambua haki, wajibu na wakumfikishia kero zako

WATUMIAJI wa huduma za umeme, mafuta, gesi na maji katika kutumia bidhaa hizo, wanakutana na matatizo, je wanafahamu kuwa wana mtetezi au chombo cha kumfikishia kilio chao?

Yupo wa kuwasikiliza ni Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), anasema Kaimu Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Stella Lupimo.

Anasema mteja au mtumiaji wa huduma za nishati na maji ni yeyote, kiwe kikundi cha watu, taasisi au kiwanda kinachotumia umeme, mafuta, gesi na maji ambazo zinazodhibitiwa na EWURA.

Anakumbusha kuwa huduma hizo zinadhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Lakini, Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, anaeleza kuwa huenda wateja wengi hawajui mahala pa kuwasilisha malalamiko yao au tatizo linapotokea.

Katika mahojiano na Nipashe, hivi karibuni jijini Dar es Salaam, anasema mara nyingi ukiwauliza watumiaji kwanini wamepata tatizo lakini hawajawasilisha malalamiko yao kuhusu huduma, wengine wanajibu wanamwachia Mungu.

Anawakumbusha wateja au watumiaji kuwa wanayo haki ya kupata huduma bora na kwa uhakika au kuhudumiwa kwa wakati na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Anataja huduma hizo kuwa ni pamoja na umeme, mafuta, gesi za kupikia majumbani pamoja na maji.

"Mtumiaji anayo haki ya kupata huduma hizi kwa kuzingatia bei halali zilizoidhinishwa na EWURA na watoa huduma kama vile mamlaka za maji, TANESCO. Wauzaji wa mafuta na gesi hawana budi kutoa huduma hizi bila upendeleo," anasema.

Stella anasema kwa mfano, Dar es Salaam, wateja wanatarajia kupata maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) bila kukatika.

KUPATA TAARIFA

Stella anazungumzia mawasiliano na wateja akisema wanapaswa kupewa taarifa sahihi kuhusu upatikanaji wa huduma wanazopata pamoja na bei zake.

Kwa mfano, watumiaji wa gesi wanapaswa kufahamu bei halisi ya gesi (LPG) iliyo kwenye mitungi kulingana na uzito na wanapaswa kupewa taarifa kuhusu mabadiliko ya bei kwa wakati.

Aidha, anasema watoa huduma wanapaswa kuwapatia watumiaji nakala ya mkataba wa huduma kwa wateja kama njia mojawapo ya kuwaelimisha haki zao wanazopaswa kupata toka kwa watoa huduma.

### USALAMA/FARAGHA

Kaimu Katibu Mtendaji wa UWURA CCC, anasema, kila mtumiaji wa huduma ana haki ya usalama na faragha, pale anapoihitaji anapaswa kupewa faragha yake na kuhifadhiwa siri kwa anachokitoa liwe lalamiko au kutoridhishwa na huduma au bidhaa.

Halikadhalika anasema anayo haki ya kulindwa kutokana na bidhaa, michakato au huduma ambazo ni hatari kwa afya au maisha. Hivyo mtoa huduma anapaswa kujiridhisha kila wakati kuwa huduma anayopeleka kwa mtumiaji ni salama na haihatarishi usalama wa mtumiaji.

Pamoja na hayo anayo haki ya kuchagua huduma kwa kuzingatia bei na ubora ili aweze kupata bidhaa inayostahili. Haki hii pia inategemea upatikanaji wa taarifa sahihi kuhusu huduma inayotolewa na watoa huduma.

Anazungumzia kusikilizwa, akisema ni haki za msingi, kusikilizwa anapowasilisha malalamiko au hoja zake kwa huduma.

Anawaambia watoa huduma kuwa ni makosa kumpuuza mteja au kutojali mahitaji yake kwa namna yoyote ile.

### KUFIDIWA HASARA

Stella anaongeza kuwa mteja anayo haki ya kufidiwa endapo atadhurika na huduma au atahudumiwa chini ya viwango vilivyowekwa na EWURA.

"Kwa mfano, kanuni ya 18 (14) ya kanuni za ufungaji umeme za mwaka 2022 zinataja kuwa TANESCO italazimika kumfidia mteja ikiwa itasababisha hatari kwake kwa kufunga miundombinu ya umeme kwa uzembe."

Halikadhalika anawaeleza wateja kuwa wana haki ya kushiriki katika mchakato wa maamuzi yanayohusu huduma za nishati na maji.

Anafafanua kuwa masuala haya yanaweza kuhusu mbadiliko ya bei ya bidhaa, kama maji na umeme na hii inamwezesha kutoa maoni yake ili kuhakikisha bei au huduma zinakuwa rafiki na endelevu kwake.

"Haki za mtumiaji wa huduma za nishati na maji ni msingi muhimu wa kuhakikisha huduma bora, usalama, na uwazi. Kuzingatiwa kwa haki hizi kunahakikisha wananchi wanapata huduma wanazostahili na kuwa na sauti katika maamuzi yanayohusu huduma hizo." Anasema Stella.

Anawaambia wanaotoa huduma hizo kuwa ni jukumu lao kuheshimu na kutekeleza haki hizo ili kufikia ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla.

### WAJIBU WA MTUMIAJI

EWURA CCC inaamini kuwa kila palipo na haki ni pia kuna wajibu. Hivyo mteja wa nishati ana wajibu wa kutekeleza ili kufikia ufanisi, anakumbusha Stella.

Anaanza na kulipa bili za huduma kwa wakati, akisema mteja anawajibika kulipa bili zake hususani kwa huduma za maji na umeme, kwa wakati mara apatapo ankara za mwezi.

Anaongeza kuwa inafanikisha uendeshaji endelevu wa huduma hizo, kwa mfano, Kanuni ya 51(1) ya Kanuni za Maji za mwaka 2020 zinamtaka mtumiaji wa maji kulipa bili yake ndani ya siku 30 tangu tarehe aliyopokea bili yake.

Wajibu wa kuhakikisha miundombinu ya huduma za nishati na maji inahifadhiwa vizuri ili kuzuia uharibifu usiohitajika ni jukumu lake pia, anasema Kaimu Katibu Mtendaji wa UWURA CCC.

"Katika hili, inashauriwa kuwa mteja anapaswa kutoa taarifa punde aonapo uharibifu wa miundombinu au anapoona mtu anaharibu miundombinu ya nishati au maji ili hatua stahiki zichukuliwe na mtoa huduma."

Mtumiaji ana wajibu wa kutoa taarifa sahihi kwa mamlaka anapogundua kuwa kuna kasoro katika huduma aliyopatiwa au unapobaini uharibifu wa miundombinu ya huduma, ili mamlaka zichukue hatua kulingana na taarifa.

### MALALAMIKO

Ingawa mtumiaji anayo haki kufidiwa au kutatuliwa changamoto anazoweza kupata kutoka kwa mteja, ni wajibu wake wa msingi kulalamikia dosari hizo. Mtumiaji ana wajibu wa kutoa maoni na malalamiko kwa njia sahihi, kama vile kupitia vituo vya huduma kwa wateja, EWURA CCC au kwenda kwa EWURA moja kwa moja, ili kusaidia kuboresha huduma au kutatua changamoto husika.

Kutumia huduma kwa usalama na uadilifu ni wajibu mwingine, akishirikiana na vyombo vya usalama kuzuia wizi wa huduma kama vile kujiunganishia umeme kienyeji au kuiba maji kutoka kwenye mabomba, kwa mfano, kutoa taarifa kwa polisi kuhusu matukio ya wizi wa umeme au maji.

Anasema kwa kuzingatia umuhimu wa haki na wajibu katika matumizi ya huduma za nishati na maji, ni muhimu kwa kila mteja kuelewa na kutambua wajibu na haki zao ipasavyo.

Haki za mtumiaji, kama vile kupata huduma bora na za uhakika, kupata taarifa sahihi na haki ya kufidiwa zinahakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi mahitaji na viwango vilivyowekwa.

Kwa upande mwingine, wajibu wa mtumiaji, kama vile kulipa bili kwa wakati, kuhifadhi miundombinu, na kutoa taarifa sahihi za matatizo, ni muhimu katika kudumisha utendaji bora na utoaji kwa ufanisi wa huduma hizo.

Anasema: "Kwa kuzingatia pande zote za haki na wajibu, tunaweza kuhakikisha kuwa huduma za nishati na maji zinakuwa salama, bora na zinazoweza kutegemewa kwa ustawi wa jamii na maendeleo ya taifa kwa ujumla." Anasema Stella.



Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji Huduma Temeke, Neema Swagara, akitoe elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Saku kuhusu matumizi sahihi ya maji, umeme na gesi ili kupeleka elimu hiyo nyumbani kwa wazazi. **PICHA: MWANDISHI WETU**



# Wafanyabiashara wa vitunguu waonywa matumizi ya rumbesa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAFANYABIASHARA wa Soko la Kimataifa la Vitunguu Misuna lililoko Manispaa ya Singida wametakiwa kufuata sheria za vipimo kwa kuachana na ujazo wa rumbesa ambao umepigwa marufuku na serikali.

Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wafanyabiashara wa soko hilo kwenye uzinduzi wa msimu mpya wa soko la vitunguu mwaka huu.

Alisema kila mfanyabiashara katika soko hilo ana wajibu wa kuzingatia ujazo wa magunia ambao unazingatia sheria za vipimo, ili kuondoa malalamiko mengi kutoka kwa wakulima na wafanyabiashara wanaotoka mikoa mbalimbali na nje ya nchi.

Alieleza ujazo unaotakiwa na unaokubalika ni kuwa kila gunia liwe na uzito usiozidi kilo 100, lakini kumekuwa na malalamiko mengi baadhi ya wafanyabiashara wanazidisha ujazo hadi kilo 120 kwa gunia moja.

Kiaratu alisema wataendelea kushirikiana na wafanyabiashara hao kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili katika soko hilo.

Aidha, aliongeza kuwa serikali inaendelea kuweka mikakati ya kuriboresha soko hilo kwa kujenga miundombinu mipya ya soko ili kuweka mazingira mazuri ya kufanyia biashara.

Naye Kaimu Meneja Wakala wa Vipimo Mkoa wa Singida, Willey Amos, alisema kuweka uzito uliopiliza kwa mazao ya kilimo ni kukiuka sheria, hivyo mtu huyo anaweza kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Alisema adhabu ambayo mtu anaweza kukumbana nayo kwa kuongeza uzito zaidi ya kilo 100 ni faini ya hadi Sh. milioni tano hali inayoweza kusababisha mfanyabiashara kupoteza mtaji wake.

Baadhi ya wafanyabiashara waliozungumza na Nipashe walisema wanakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo suala vipimo kuwa vikubwa kupita kilo 100 na wakati mwingine ujazo unakuwa chini ya kilo 100.

Walitaja changamoto nyingine ni kudaiwa ushuru katika kila geti wanalopita hata kama wamelipa ushuru kwa kufuata sheria na taratibu.

**Aidha, aliongeza kuwa serikali inaendelea kuweka mikakati ya kuriboresha soko hilo kwa kujenga miundombinu mipya ya soko ili kuweka mazingira mazuri ya kufanyia biashara.**

# Watanzania watolewa hofu ujio teknolojia akili bandia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa matumizi ya Teknolojia ya Akili Bandia (AI) hayatasababisha Watanzania kupoteza ajira kwa kuwa ni njia ya fursa nyingi za ajira.

Mkurugenzi wa Tume ya TEHAMA nchini (ICTC), Dk. Nkundwe Mwasaga, aliyasema hayo jana mkoani hapa na kuwatoa hofu Watanzania kuhusu dhana hiyo.

Alisema pamoja na teknolojia hiyo kufanya shughuli za kibinadamu lakini haiwezi kusababisha Watanzania kupoteza ajira.

Alisema kinachopaswa kuzingatiwa ili kulinda ajira ni uhuishaji wa maarifa binafsi katika matumizi ya teknolojia hiyo.

"Nimesikia watu wengi wakizungumzia jambo hilo moja la kuvutia la teknolojia hii mpya, kuna watu ambao wanapenda soko la hofu na kuna wanaoenda kufanya biashara ya hofu kuhusu teknolojia."

"Lakini AI imekuja kumsaidia mwanadamu mtaalamu ili aweze kuwa na tija zaidi kwa hivyo tunaamini kuwa AI itatufanya kuwa na ufanisi zaidi katika suala la utoaji wa huduma katika suala, ubora wa uamuzi ambao tunafanya katika suala, uwezo wa kuzalisha vitu vya ubora wa juu," alisema. Aidha, alibainisha kuwa zipo faida nyingi katika kuwekeza kwenye akili bandia ikiwamo kukuza uzalishaji na ufanisi na kukuza uchumi na ubunifu.

Alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na McKinsey nchini Uingereza, inakadiriwa akili ya bandia inayozalishwa inaweza kuongeza Pato la Taifa la Uingereza kutoka Dola za Marekani Trilioni 2.6 hadi 4.4 kwa kulinganisha na mwaka 2021 iliyokuwa Dola za Marekani trilioni 3.1.

Mtaalamu wa uchumi kutoka Kampuni ya IBM, Martin Fleming, alisema uwepo wa akili bandia hautaondoa kazi za watu bali utabadili namna ya ufanyaji kazi.

Profesa wa uchumi wa kazi kutoka Chuo Kikuu cha Buffalo Marekani, Joanne Song McLaughlin, alisema kazi nyingi bila kujali tasnia zina vipengele ambavyo vina uwezekano wa kuendeshwa kiteknolojia.

Ripoti iliotolewa Machi 2023 kutoka Goldman Sachs inakadiria kwamba akili bandia yenye uwezo wa kutengeneza maudhui inaweza kufanya robo ya kazi zote zinazofanywa na binadamu kwa sasa.



Katibu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Nkuhungu jijini Dodoma akizungumza na waandishi wa habari kuhusu jamii kutoa kipaumbele cha malezi kwa watoto wa kiume ili kuwaondoa kwenye hatari ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia jana kanisani hapo. **PICHA: PAUL MABEJA**

# 'Wakristo tumieni mwezi wa Kwaresma kujitathmini'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKRITO nchini wametakiwa kuutumia mwezi wa Kwaresma kujitathmini na kuacha kufanya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto, wanawake na wazee, ambavyo vinaendelea kuongezeka kila siku katika familia na maeneo ya kazi.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Nkuhungu jijini hapa, Mwamini Mwanjisi wakati wa ibada maalum ya uchangiaji wa ujenzi wa kanisa kwa waumini waliozalwa Februari.

Alisema hivi sasa nchini vitendo vya ukatili vinaendelea kuongezeka kutokana na watu kukosa hofu ya Mungu, hali inayosababisha kuwapo matukio ya uovu ndani ya familia na jamii kwa ujumla.

"Ukatili hivi sasa umeongeza ndani ya ndoa, kazini na hata kwa wadada wa kazi. Watu wanafanya mambo mabaya hayana kabisa hofu ya Mungu, hivyo katika kipindi hiki cha mwezi wa Kwaresma lazima tushiriki mateso ya Yesu na kujitathmini ili kuacha ukatili huu ambao ni dhambi mbele za Mungu wetu," alisema.

Naye Mratibu wa Vijana Kanisa la KKKT Dayosisi ya Dodoma, Mchungaji Victoria Ntenga, alisema kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya ukatili nchini serikali inapaswa kushirikiana na viongozi wa dini kukomesha hali hiyo.

"Moja ya ukatili ni ndoa za utotoni kwa watoto wetu wa kike ambao wamekuwa wakiozeshwa na watu ambao siyo umri wao na wengine kunyimwa haki yao ya kupata elimu.

"Hivyo basi suluhu ya suala hili la ndoa za ututoni ni mabadiliko ya sheria ya ndoa ili kuleta sheria itakayobainisha umri mkubwa wa mtoto wa kike kufunga ndoa tofauti na ilivyo sasa," alisema.

Alisema ndoa za utotoni ni ukatili, hivyo wanawake nchini wanapaswa kushikamana, kupambana na hali hiyo badala ya kuwaachia viongozi wa dini au serikali peke yake.

"Ndoa za utotoni ni ukatili mkubwa sana wanawake, hivyo ni lazima tushikamane kutetea haki za watoto wetu wa kike umri wa mtoto kuolewa kwenye sheria yetu ni mdogo sana, lazima ije sheria ambayo itasaidi kubadili hilo," alisema

Katibu wa Kanisa la KKKT Usharika wa Nkuhungu, Benjamini Mdadi, alisema pamoja na jitihada zinazofanywa kumtetea mtoto wa kike ipo haja ya kumwangalia mtoto wa kiume pia.

Alisema hivi sasa uwekezaji mkubwa umefanywa kwa mtoto wa kike hali ambayo imesababisha mtoto wa kiume kuachwa na kumweka katika hali ya hatari zaidi.

Mwenyekiti wa umoja wa waumini waliozaliwa Februari, Emmanuel Nalogwa, alisema badala ya kusherehekea sikukuu za kuzaliwa nyumbani na familia zao wameona ni vyema washiriki kuchangia ujenzi wa kanisa.

Alisema katika michango yao ya vitu mbalimbali wamefanikiwa kuchangia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa kanisa hilo ambalo bado halijakamilika.





# Waomba kupatiwa elimu ya uhifadhi wa maliasili kuepuka migogoro na wanyama

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAJASIRIAMALI wanaofanya shughuli zao kwenye maeneo ya shoroba za hifadhi za taifa, wamewaomba wataalamu wa uhifadhi wa mazingira na maliasili kwenda kuwapatia elimu ya uhifadhi wa maliasili kwenye maeneo hayo, ili kuepuka migogoro kati yao na wanyamapori.

Walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya kwenye mkutano wa wadau wa sekta ya umma na binafsi kuhusu uwekezaji endelevu na kudhibiti biashara haramu ya wanyamapori ambazo zimekuwa zikiathiri hifadhi.

Vilevile mkutano huo ulilenga kudhibiti migogoro ya binadamu na wanyamapori kwenye ushoroba wa Ruaha-Rungwa-Katavi ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara na kuathiri shughuli za uhifadhi.

Evaluna Kivunjabei ambaye ni mfugaji wa nyuki katika Kata ya Mafyeko wilayani Chunya, alisema mafunzo yanayohusu masuala ya uhifadhi wa maliasili yanatakiwa kutolewa kwenye maeneo ya wananchi badala ya mjini.

Alisema katika eneo analotoka wapo wafugaji wengi wa nyuki na wajasiriamali wa mazao ya nyuki ambao wanafanya shughuli zao kwenye maeneo ya hifadhi, lakini hawana elimu ya kutosha kuhusu uhifadhi wa maliasili.

"Tunaomba wataalamu wawe wanatufuata vijijini ambako tunafanyia shughuli zetu, kule ndiko waliko wajasiriamali wengi zaidi, sisi tutafikisha elimu hii kwa wenzetu lakini wakija wao wenyewe wataalamu ni vizuri zaidi," alisema Evaluna.

Upendo Christian alisema anafanya shughuli za uzalishaji wa asali kwenye mapori mbalimbali yaliyoko katika Kata ya Gwala wilayani Songwe.

Alisema wamekuwa wakifanya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na kwamba baadhi ya wajasiriamali hawana uelewa wa kutosha kuhusu uhifadhi wa maliasili hali ambayo imekuwa ikiwafanya wafanye mambo ambayo hayastahili kwenye uhifadhi.

Meneja Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi wa mradi wa USAID-Tuhifadhi Mazingira, Dk. Elikana Kalumanga, alisema lengo la mradi huo ni kuokoa shoroba mbalimbali ambazo zimevamiwa na binadamu na kuanza kuathiri shughuli za uhifadhi.

Alisema wanaendelea kujenga uwezo kwa wadau wa sekta binafsi ili na wao washiriki kwenye shughuli za uhifadhi kama ilivyo kwa sekta za umma.

"Tunafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa nchi nzima yapo maeneo 61 ya shoroba ambayo yameainishwa na kwa Mkoa wa Mbeya yapo maeneo saba," alisema Dk. Kalumanga.

Mwakilishi wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Deogratius Massawe, alisema shoroba nyingi zina hali mbaya kutokana na uwekezaji unaofanyika kwenye maeneo hayo kutokuwa endelevu.

Alisema wajasiriamali wengi wanaofanya shughuli zao kwenye maeneo hayo hawana elimu ya kutosha kuhusu uhifadhi hali ambayo inasababisha waharibu maliasili zilizopo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwataka wadau kutoa elimu ya kuzuia uwindaji haramu wa wanyamapori kwenye hifadhi za taifa ili kulinda maliasili hizo.

Alisema maliasili zilizomo kwenye hifadhi mbalimbali za taifa ni muhimu kwa ajili ya kuimarisha shughuli za utalii na kuongeza mapato yatokanayo na sekta hiyo.



Maofisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mbeya, wakitoa elimu kwa wanafunzi kuhusu matumizi ya mtungi wa hewa ya oksijeni wakati wa mafunzo ya uokozi, mafunzo hayo yalitolewa hivi karibuni kwenye ofisi za jeshi hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Soko Kuu la Njombe lafungwa taa, wafanyabiashara kicheko

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAFANYABIASHARA wa Soko Kuu la Halmashauri ya Mji Njombe mkoani Njombe, wameishukuru serikali kwa kutatua kero zao mbalimbali ikiwamo uhafifu wa taa ambao ulikuwa ukisababisha kutumia tochi.

Wakizungumza katika shughuli ya usafi iliofanyika sokoni hapa, wafanyabiashara walisema hivi sasa wanafanya biashara usiku na mchana.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Bruno Mgima, alisema hapo awali ilikuwa ikifika usiku wanalazimika kutumia taa zao binafsi kutokana na uhafifu wa mwanga wa taa zilizokuwapo.

"Taa zilizokuwa zimefungwa wakati soko linafunguliwa pamoja na miundombinu ya vyoo vilikuwa vinakosa maji lakini kwa sasa kero zetu nyingi zinaendelea kutatuliwa, tunawashukuru viongozi wa soko ambao wanapambana usiku na mchana," alisema Mgina.

Naye Alex Makao alisema ili kero zitatuliwe kwa wakati viongozi wanapaswa kuwa karibu na wafanyabiashara ili kuzitambua na kuzifanyia kazi kwa haraka.

Mwenyekiti wa Soko Kuu la Njombe, Athan Kyando, aliwashukuru viongozi wote kwa kuwa sehemu ya utatuzi wa kero mbalimbali za wafanyabiashara.

Aliongeza kuwa: "Tunashukuru viongozi wa mkoa kwa kutatua changamoto za uhaba wa maji, uboreshaji wa gari la kubeba taka ambalo kwa sasa linafika kwa wakati kwani soko hili la kisasa limekuwa sehemu ya utalii hapa mkoani kwetu."

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Njombe Mji, Kuruthum Sadick alisema halmashauri hiyo ilijiwekea utaratibu wa kufanya usafi kila mwisho wa mwezi kama ilivyo maeneo mengine nchini.

Alisema zoezi la usafi katika Soko Kuu la Njombe unafaida kubwa kwa wafanyabiashara pamoja na wateja wanaokuja kununua bidhaa ikiwamo kuwaepusha na magonjwa ya mlipuko.

Katibu Tawala Wilaya ya Njombe, Agatha Mhaiki aliushukuru uongozi wa soko kwa kuwasilisha kero za wafanyabiashara ambazo baadhi zinaendelea kupatiwa majibu na viongozi wa mkoa.

Mbunge wa Njombe, Deo Mwanyika, alisema kwa kiasi kikubwa kero za wafanyabiashara zimeshughulikiwa kwa asilimia 80.

"Kwa zaidi ya asilimia 80 changamoto zenu imeambiwa zimetatuliwa ni jambo jema kwa sababu kero na changamoto sasa zimepungua, bado kero ya maji haijatatuliwa kwa kiasi kikubwa katika soko hili lakini tunaahidi kuzimaliza kero zote," alisema Mwanyika.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliwapa heshima kwa kutujengea soko hilo kubwa lenye hadhi ya kimataifa na hivyo Mkoa wa Njombe utapiga hatua kwenye uchumi.

## Wawekezaji waitwa kuwekeza hekta 297,925 Njombe

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

SERIKALI wilayani Ludewa mkoani Njombe imewaomba wawekezaji nchini kujitokeza kwa ajili ya kuwekeza kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 297,925 ambalo ni sawa na 66% linalofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali.

Wito huo umetolewa katika kikao kazi cha wadau wa kilimo kilichofanyika wilayani hapa kikiwa na lengo pia la kutangaza fursa zinazopatikana.

Ofisa Kilimo Wilaya ya Ludewa, Godfrey Mlelwa, alisema wilaya hiyo ina jumla ya hekta 465,030 zinazofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali hadi hivi sasa hekta 167,105 sawa na asilimia 34% pekee ndizo zinazolimwa na kubakiwa na ziada hiyo ya hekta 297,925.

"Wilaya imegawanyika katika kanda tatu za uzalishaji ambazo ni ukanda wa juu, ukanda wa kati na ukanda wa chini na mazao ya biashara yanayostawi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ni kahawa, parachichi, chai, pareto, korosho na alizeti," alisema Mlelwa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva, alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akihimiza uboreshaji katika sekta ya kilimo kwa vitendo, ambapo kwa Wilaya ya Ludewa ametoa pikipiki 58 kwa ajili ya maofisa ugani ili waweze kuwafikia wakulima kwa urahisi.

Mwanziva alisema serikali imejizatiti kuhakikisha kwamba wakulima wanapata pembejeo kwa wakati sambamba na kuimarisha masoko.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sunday Deogratius, alisema pamoja na kuhitaji wawekezaji katika kilimo pia wanahitaji mazao yanayozalishwa wilayani hapa yaweze kuongezewa thamani.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ludewa, Gervas Ndaki, alisema kwa mujibu wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho ya mwaka 2020/2025 Ibara ya 37 imeeleza kuwa katika kipindi cha miaka mitano chama hicho kitasimamia mapinduzi katika sekta ya kilimo na kuhakikisha kinakuwa kilimo chenye tija na kinachotumia teknolojia ya kisasa.

Mmoja wa wakulima, Christopher Mgimba, aliipongeza serikali kwa kuchukua hatua za haraka za kutokomeza wadudu aina ya viwavijeshi mashambani.



## Serikali kufufua uzalishaji, usafirishaji mazao ya viungo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesema imejipanga kurudisha hadhi ya Zanzibar ya miaka 1960 ya kuongoza kwa uzalishaji na usafirishaji nje ya nchi mazao ya viungo.

Hatua hizo ni pamoja na kuwashajihisha wakulima kulima mazao hayo kwa kuwapatia mbinu mbalimbali za kisasa pamoja na kuwapatia mbegu zinazokwenda na wakati kwa soko la sasa.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis wakati akijibu swali la nyongeza lililoulizwa na mwakilishi wa Bumbwini, Mtumwa Peya Yussuf aliyetaka kujua mikakati ya wizara katika kuwasaidia wakulima kulima mazao ya viungo.

Waziri huyo alisema mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kurudisha hadhi ya Zanzibar ya miaka ya nyuma kuongoza kwa uzalishaji wa bidhaa za viungo.

Shamata alisema uzalishaji wa mazao ya viungo umeshuka kufuatia baadhi ya maeneo mengi ikiwamo yenye rutuba kutumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kudumu za wananchi.

Alisema Zanzibar ilikuwa maarufu kwa uzalishaji wa bidhaa za viungo ikiwamo pilipili manga, uzile pamoja na hiliki ambazo zimekuwa zikisafirishwa nje ya nchi.

Alisema kwa sasa zao la vanila limeonesha kupata mafanikio makubwa huku bei yake katika soko la dunia ikipanda juu.

Waziri huyo alisema wizara kwa kushirikiana na idara ya kilimo wameanza kuwasaidia wakulima na kuwapa mbinu za kisasa katika kulima zao la vanila.

Alisema: "Mh. Spika tumeanza kazi ya kuwasaidia wakulima kwa kushirikiana na idara ya kilimo, kwanza tumeanza kuwahamasisha wakulima wetu kujikita katika kilimo cha vanila chenye tija kubwa na bei yake nzuri soko la dunia."

# Kampuni ujenzi wa barabara yapewa onyo ubabaishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa onyo kwa Kampuni ya MECCO inayojenga Barabara ya Chakechake-Wete Pemba (22.1) kuhakikisha inakamilisha ujenzi huo kwa wakati na kuacha kutoa visingizio ambavyo havina sababu.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadir Abdulatif Al-Wardi wakati akitoa ufafanuzi kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Nadir alisema mkataba wa ujenzi wa barabara hiyo upo na unafahamika ambao umeweka mambo yote ya msingi.

Alisema hakuna sababu kwa Kampuni ya Mecco kuchelewesha ujenzi huo na kujenga barabara kwa njia ya kusuasua kwa sababu mambo yote yamewekwa sawa ikiwamo malipo ya kazi za ujenzi.

Alisema kwamba mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kujenga barabara katika Kisiwa cha Pemba kwa njia ya lami na kwa ubora, lengo likiwa ni kukifungua kisiwa hicho katika miundombinu ya mawasiliano.

Aidha, alisema Barabara ya Chakechake hadi Wete (Km 22.1) ni ya kimkakati ambayo kukamilika kwake inakwenda kuunganisha mikoa miwili ya Pemba katika miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami.

"Barabara ya Chakechake hadi Wete ni barabara ya kimkakati ambayo imetajwa katika mpango wa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025, hivyo kitendo cha kuchelewesha ujenzi wake ni kuturudisha nyuma katika malengo yetu," alisema.

Naibu waziri huyo alisema serikali inafuatilia mwenendo wa ujenzi wa barabara hiyo ambao ulianza Februari mwaka 2022 na unatarajiwa kumalizika.



Mbunge wa Jimbo la Mfenesini Wilaya ya Magharib A Unguja, Zubeda Khamis Shaibu, akimkabidhi jiko la gesi mmoja wa wananchi wa jimbo hilo jana, alitoa majiko 130 ili kuachana na matumizi ya kuni na mkaa na kulinda mazingira. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mbunge ahimiza uhifadhi mazingira kuepuka athari tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MBUNGE wa Mfenesini, Zubeda Khamis Shaibu, amewataka wananchi kulinda na kuhifadhi mazingira ili kuepukana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Aliyasema hayo jana wakati akikabidhi majiko ya gesi kwa wajumbe wa CCM wa Mfenesini ikiwa ni miongoni mwa harakati za kuunga mkono hatua ya Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi katika kulinda mazingira.

Alisema majiko hayo yatasaidia kupunguza matumizi ya kuni na mkaa wakati wa kupika chakula ambapo miongoni mwa uharibifu wa mazingira ni ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

Alisema umefika wakati kwa wananchi kuacha matumizi ya nishati ya kuni na mkaa ili kuinusuru nchi na majanga ya athari za kimazingira.

Aidha, alisema matumizi ya kuni na mkaa hayaathiri hali ya kimazingira pekee, lakini huathiri afya za wananchi hasa wanawake ambao ndiyo waathirika zaidi.

"Moshi unaotoka na kuni ni hatari kwa afya za wananchi, unamkuta mama macho mekundu kwa moshi na wengine hufikia kuitwa wachawi kwa sababu ya macho yao kubadilika rangi kwa sababu moshi umeshawaathiri," alisema.

Hata hivyo alisema ukataji wa miti na uharibifu wa misitu unachangia ukosefu wa mvua na uwepo wa hali ya joto kali.

Alizema Zanzibar ni kisiwa kama hakutakuwa na juhudi za ziada za kupunguza makali ya athari za mabadiliko ya tabianchi kitaangamia, hivyo ni vyema kila mmoja kuchukua juhudi za makusudi ya kulinda na kuhifadhi mazingira.

Mbunge huyo alisema utoaji wa majiko hayo ya gesi hautoishia kwa wajumbe hao wa CCM bali yatawafikia hadi baadhi ya mama lishe katika jimbo hilo, ili kupunguza na kuacha kabisa matumizi ya kuni na mkaa.

Wajumbe waliokabidhiwa majiko hayo walisema kuwa elimu zaidi inahitajika kwa wananchi kuhusu matumizi ya nishati mbadala ya kupikia ili kulinda na kuhifadhi mazingira.

Mwatumu Bakari ni miongoni mwa wajumbe hao alisema nishati ya gesi ni rafiki katika utunzaji wa mazingira lakini bado baadhi ya wananchi wanauwoga na hofu wa kutumia nishati hiyo.

"Bado wapo wananchi wanaogopa kutumia gesi kwa kupikia na hii inatokana na kutokua na uelewa wa matumizi yake," alisema.

Verenika Ndaro, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mfenesini, alisema matumizi ya nishati mbadala ikiwamo gesi kwa ajili ya kupikia kuokoa muda kwa wanawake badala ya kuchukua muda mrefu kutafuta kuni.

Alisema Jimbo la Mfenesini ni mwathirika wa athari za kimazingira kwa ukataji wa miti jambo ambalo ni hatari kiuchumi, kijamii na kisiasa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**FARIDA MJILI MGUDE** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria **(Passport) yenye namba TAE300720** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 11/02/2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBD/RB/475/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**REGINALD NDINDAGI KWIZELA** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE246862** iliyotolewa uhamiaji makao makuu mnamo tarehe 26/11/2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/26835/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**PAUL CHARLES MSABILA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.359/0342** kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia **KIGURUNYEMBE SECONDARY SCHOOL** mwaka 1996. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/26767/2024**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ALLY HARUNA CHUMA,** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YAKE YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA **TAE039848** ILIYOTOLEWA TAREHE 25/07/2018 NA IDARA YA UHAMIAJI DAR ES SALAAM. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DAR/ILA/26756/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MBWANA MOHAMED MWAKIVUMBI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0340/0131** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **POPATLAL SECONDARY SCHOOL** mwaka 1985 . kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/TAN/TSN/1397/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**David Mahende Mahiti** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki YENYE NAMBA YA USAJILI **MC 325 DPG** aina ya **sanlg** yenye chassis No **LBRSPJB56NZ035230** NA ENGINE NO **SL157FM122941376.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.TAARIFA YA POLISI: **KAH/TR /RB/211/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ENDRISHA MUSSA NASSORO,** Anatangaza kupotea kwa Kadi ya gari Aina ya **TOYOTA CROWN** Yenye no za Usajili **T291DRL** Yenye CHASSIS NO **GRS1800014404,** ENGINE NO **4GR0025378.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/5556/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PHINIAS MEWANYA NYAMOHINYA** anatangaza kupoteza Kwa kadi ya gari aina ya ISUZU yenye usajili Namba **T 201AMN,** model HTR model Number **HTR114-31P** Chassis no **2206263** Engine no, **421469.** Kwa yeyote aliyeiona atoe taarifa kituo Cha polisi kilichokaribu.
Taarifa ya Polisi **TAR| RB|608|2023.**

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1278 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE AHAZI ASUMILE KAJUNI**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY TUNSUBILEGE ANDONDILE MBWILE..........PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above – named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 12th day of March, 2024.

DATED at KYELA this **26th day of February, 2024.**

DISTRICT COURT KYELA TANZANIA

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE I/C KYELA.

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE KYELA

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 2945 OF 2024**

In the Matter of the Estate of the Late: **REHEMA SALVATORY KASEMBE**

**By 1: ERNEST ANTHONY SAMBILA.**
**2: ______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the M. KALLOMO day of **29/02/2024**
Dated at.....this **22 day of 02.2024**

RESIDENT MAGISTRATE

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TARIME**

**MAOMBI MADOGO NA. 192 YA 2023**

**1.DAUDI MGENDI NTUMBO**
**2.ELIZABETH DAUDI NTUMBO.............WALETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**GEOFREY CHACHA MANKO....................MJIBU MAOMBI**

**KWA: GEOFREY CHACHA MANKO – POPOTE ULIPO**

Fahamu kwamba waleta maombi **DAUDI MGENDI NTUMBO NA ELIZABETH DAUDI NTUMBO** wameleta maombi madogo Na. 192/2023, dhidi yako. Hivyo basi kama unakusudia kupinga maombi hayo unatakiwa kuleta majibu yako na uwepo barazani wewe binafsi, wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria, tarehe 15/03/2024, siku ambayo shauri limepangwa kutajwa.
Endapo hutatekeleza hayo, shauri litaendelea upande mmoja dhidi yako na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe **16/02/2024**

MAHELELE.M.S

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) TARIME.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO, KITUO CHA MJINI**

**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...12/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**

**MAREHEMU: ISLAM ABED wa K/NDEGE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SAADI ISLAM ABED**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 03 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 23 mwezi 02 mwaka 2024

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,
KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA



Mkuu wa Mpango wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa, Inger Andersen (kushoto), akiwa na mawaziri wa mazingira wa Sweden na Kenya. **PICHA: MTANDAO**

# Mauaji Gaza yamchomoa Waziri Mkuu Palestina

**GAZA,** PALESTINA

WAZIRI Mkuu wa Palestina, Mohammad Shtayyeh, amejiuzulu kutokana na kushamiri kwa ghasia katika eneo la Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kwa mabavu na Israel na kuendelea kwa vita vinavyosababisha mauaji ya halaiki huko Ukanda wa Gaza.

Hayo ni kwa mujibu wa barua iliyowasilishwa na waziri huyo jana kwa Rais wa Palestina Mahmoud Abbas, ikieleza kwamba uamuzi huo umetokana na ongezeko kubwa la vita ambalo halijawahi kushuhudiwa katika Ukingo wa Magharibi, vinavyosababisha njaa na mauaji ya halaiki katika Ukanda wa Gaza.

"Ninaona kwamba hatua inayofuata na changamoto zake zinahitaji mipango mipya ya kiserikali na kisiasa ambayo inazingatia ukweli mpya wa Gaza na haja ya makubaliano kulingana na umoja wa Palestina na upanuzi wa umoja wa mamlaka juu ya ardhi ya Palestina," alisema.

Pia ilibainishwa kuwa hatua hiyo ya Shtayyeh imekuja wakati shinikizo la Marekani likiongezeka kwa Rais Abbas kuitikisa Palestina na kuanza kufanyia kazi muundo wa kisiasa ambao unaweza kutawala taifa hilo kutokana na vita.

Aidha, inaelezwa kuwa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu mara nyingi amekataa wito wa Rais Abbas kuchukua udhibiti wa taifa la Palestina na kuitawala Gaza.

Ilielezwa kuwa wiki iliyopita, wabunge wa Israel waliunga mkono hatua hiyo ya Waziri Netanyahu kukataa kwa kutambua taifa la Palestina.



"Kulikuwa na jaribio la kutulazimisha kuanzishwa kwa taifa la Palestina ambalo sio tu kwamba lingeshindwa kuleta amani lakini lingehatarisha taifa la Israel," alisema Netanyahu.

Hata hivyo, Wizara ya Mambo ya Nje ya Palestina ilikashifu kura hiyo na kuishutumu Israel kwa kushikilia haki za Wapalestina kutokana na kukalia kwa mabavu ardhi za taifa hilo.

"Wizara inathibitisha kwamba uanachama kamili wa Jimbo la Palestina katika Umoja wa Mataifa na kutambuliwa kwake na mataifa mengine hakuhitaji ruhusa kutoka kwa Netanyahu," ilisema katika taarifa.

Wakati Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) ikisikiliza takriban nchi 50 kuhusu athari za kisheria za utawala wa Israel katika Ukingo wa Magharibi wa Mto Jordan, Waziri wa Fedha wa Israel, Bezalel Smotrich,alitangaza mpango wa kujenga nyumba mpya zaidi ya 3,300 kukabiliana na risasi iliyoua. raia mmoja wa Israel.

Smotrich alisema uamuzi huo utaanza mchakato wa kuidhinishwa kwa nyumba mpya 300 katika makazi ya Kedar na 2,350 huko Maale Adumim, ambako shambulio hilo lilitokea.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken alisema amesikitishwa kusikia kuhusu tangazo la Israel la makaazi mapya.

"Imekuwa sera ya muda mrefu ya Marekani chini ya utawala wa Republican na Democratic sawa kwamba makazi mapya hayana tija katika kufikia amani ya kudumu," alisema.

"Pia haziendani na sheria za kimataifa. Utawala wetu unashikilia upinzani thabiti kwa upanuzi wa makazi na kwa uamuzi wetu hii inadhoofisha tu, haiimarishi, usalama wa Israeli," alisema.

Vile vile, inaelezwa kuwa ghasia katika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kwa mabavu zimeongezeka sana baada ya shambulio la Oktoba 7 la Hamas katika eneo la kusini mwa Israel lilioua watu 1,139. Huku Wizara ya Afya ya Palestina ikisema mashambulio ya kulipiza kisasi ya Israel huko Gaza yaliua zaidi ya watu 29,000.

Maofisa wa afya wa Palestina pia wanasema watu wasiopungua 401 wameuawa na moto wa Israel katika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kwa mabavu katika kipindi hicho. **ALJAZEERA**

## Mabadiliko ya tabianchi yaikutanisha UNEA Kenya

**NAIROBI,** KENYA

SHIRIKA la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEA) linafanya mkutano Nairobi Kenya kujadili jinsi mataifa yanavyoweza kushirikiana katika kukabiliana na migogoro kama mabadiliko ya tabianchi na kupotea kwa viumbe hai.

Kabla ya mkutano huo, Mkuu wa Mpango wa Kimataifa wa Mazingira (UNEP), Inger Andersen, alisema hakuna binadamu yeyote anayeishi peke yake na kwamba kila mtu anaishi katika sayari ya dunia ambako athari za mabadiliko ya tabianchi zinaweza kumkuta moja kwa moja.

"Kila mmoja lazima ashirikishwe kwa kuwa njia pekee ya kutatua baadhi ya matatizo hayo ni kwa mazungumzo ya pamoja," alisema.

Mkutano huo ni kikao cha sita cha Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UN) kinachohudhuriwa na nchi wanachama, mashirika ya kiraia, wanasayansi na sekta binafsi.

Katika mkutano huo, nchi wanachama hujadili rasimu za maazimio kuhusu masuala mbalimbali ambayo baraza hilo hupitisha baada ya makubaliano. **DW**

## Waumini 15 wa Kanisa Katoliki wauawa Burkina Faso

**OUAGADOUGOU,** BURKINA FASO

WAUMINI 15 wa Kanisa Katoliki Burkina Faso wameuawa na wengine wawili kujeruhiwa katika shambulio la kigaidi lililofanywa katika kanisa hilo wakati wa ibada ya Jumapili.

Inaeleza kuwa tukio hilo lilitokea katika kijiji cha Essakane kwenye jimbo la Oudalan karibu na mpaka wa Mali. Huku ofisa mmoja wa kanisa hilo akidai kuwa watu hao wenye silaha waliotekeleza shambulio hilo wanashukiwa kuwa wanamgambo wa kijihadi.

Mamlaka katika mji mkuu wa nchi hiyo ya Afrika Magharibi, Ouagadougou haijatoa tamko lolote kuhusiana na shambulio hilo. Licha ya taarifa ya mkuu wa dayosisi ya eneo hilo Abate Sawadogo, iliyobainisha kuwa watu 12 waliuawa papo hapo, huku wengine watatu wakifariki hospitalini.

"Katika hali hii chungu, tunakuomba kuwaombea waliokufa kwa imani, afueni ya haraka kwa waliojeruhiwa, na uimarishaji wa mioyo ya huzuni," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, ilielezwa kuwa hilo ni tukio baya zaidi la hivi karibuni kutokea nchini humo na kuhusishwa na wapiganaji wenye itikadi kali.

Huku ikibainishwa kwamba zaidi ya theluthi moja ya Burkina Faso kwa sasa iko chini ya udhibiti wa waasi.

Ilielezwa kuwa mamlaka nchini humo zimekuwa zikipambana na makundi ya kijihadi yenye mafungamano na al Qaida na Islamic State, ambayo yamechukua maeneo makubwa ya ardhi na kuwakosesha makazi mamilioni ya watu katika eneo la Sahel.

Katika miaka mitatu iliyopita, makanisa yamekuwa yakilengwa na waumini wengi kuuawa. Huku Rais wa Burkina Faso anayeungwa mkono na jeshi Ibrahim Traoré akibainishwa kuwa wanajeshi wa Russia wanaweza kutumwa kupambana na wanajihadi katika nchi hiyo ya Afrika Magharibi. **BBC**

# MSHINDI WA 'TIGO KILI HALF MARATHON' 2024 ATOA SIRI

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

MSHINDI wa mbio za nusu marathon za 'Tigo Kilimanjaro Half Maratho 2024', Faraja Damas, amesema siri ya ushindi huo ni kujituma na kupambania ndoto yake.

Mwishoni mwa wiki Damas aliibuka mshindi wa mbio hizo baada ya kukimbia kwa saa 01:03:33 na kumshinda Mkenya Peter Mwangi kwa sekunde 11, ambaye alitumia muda wa saa 01:3:44.

Damas ambaye ni askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), alisema ushindi huo ni furaha kubwa kwake kwa kuwa kujituma kwake na kutokata tamaa sasa kumemlipa.

Alisema tangu ameanza kukimbia mwaka 2004, amekuwa akipitia nyakati mbalimbali mpaka kufukia kushinda mbio hizo za nusu marathon zinazodhaminiwa na Kampuni ya Tigo.

"Nakumbuka mwaka 2004 nikiwa mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Ligwa iliyopo wilayani Ikungi mkoa wa Singida, nilishiriki mbio za kilomita tano zilizofanyika Babati, Manyara nikiwa 'miguu peku' na kuibuka kidedea na tangu mwaka huo nikawa na ndoto ya kuwa mwanariadha mkubwa nchini Tanzania na ninaishukuru Kampuni ya Tigo kwa kuniwezesha nikaanza kufikia ndoto yangu," alisema Damas.

Aidha, Damas alimshukuru Mungu kwa kipaji alichompa na kwamba atahakikisha anafanya vizuri zaidi siku za usoni.

"Ninamshukuru sana Mungu kwa kipaji alichonijalia kwani kasi ipo kwangu na kasi ipo Tigo 4G na ninaamini kuwa nitakwenda kuiwakilisha Tanzania vema Aprili mwaka huu Viena katika kuwania kufuzu mashindano ya Olimpiki yanayotarajiwa kufanyika jijini Paris, Ufaransa Agosti mwaka huu," alisema Damas.

Kwa upande wa wanawake katika mashindano hayo, wanariadha wa Tanzania pia waling'ara ambapo Failuna Matanga aliongoza kwa kushika nafasi ya kwanza kwa kutumia muda wa saa 1:16:54 akifuatiwa na Mtanzania mwenzake, Neema Kisuda, aliyeshika nafasi ya pili kwa kutumia muda wa saa 1:16:54. Akizungumza katika mbio hizo, Ofisa Mkuu wa Fedha wa Kampuni ya Tigo, Innocent Rwetabura, alifafanua kuwa kampuni yake imekuwa ikishiriki katika kudhamini Mbio za Tigo International Kili Half Marathon kwa mwaka wa tisa sasa, ambazo ni moja ya mbio za Kilimanjaro International Marathon zilizofikisha miaka 22 yenye mafanikio makubwa.

"Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza waandaaji wa mbio hizi kwa kuziendesha kwa weledi mkubwa na kuzifanya kuwa za viwango vya kimataifa," alisema Rwetabura.

"Tangu mwaka 2015, Tigo tumekuwa wadhamini wa mbio za kilomita 21 maarufu kama Tigo Kili International Half Marathon ili kukuza utalii wa michezo, kuibua na kukuza vipaji vya riadha na kuongeza chachu kwenye sekta ya utalii wa ukanda huu wa Kaskazini ikiwamo kuutangaza urithi wetu wa Mlima Kilimanjaro," aliongezea kusema Rwetabura.

Aidha, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, aliwapongeza wanariadha hao kwa ushindi huo ambao umeakisi matayarisho yao mazuri kuelekea kwenye mashindano ya Olimpiki.




Mwanariadha Mtanzania, Faraja Damas, akimaliza mbio za Kili Tigo international Marathon 2024, zilizofanyika Jumapili kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika Moshi na kuibuka mshindi wa kwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# New City bado yajitafuta Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LICHA ya kufanikiwa kuvuna alama nne katika michezo miwili iliyocheza ikiwa ugenini Kisiwani Pemba, timu ya New City imesema bado inahitaji kuendelea kushinda zaidi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusalia Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

New City FC katika mchezo wake wa 19 ilifanikiwa kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya wenyeji wao, Maendeleo FC wakati juzi katika mzunguko wa 20, timu hiyo ikiwa huko Pemba iliibuka na pointi tatu kwa kuifunga Chipukizi FC bao 1-0 kwenye mchezo uliochezwa Finya.

New City FC imeshinda jumla ya michezo mitano na kutoka sare saba na kufungwa mechi nane kati ya michezo 20 waliyocheza.

Kwa matokeo hayo iliyoyapata Kisiwani Pemba, New City FC sasa wamefanikiwa kujiondoa katika mstari mwekundu wa kushuka daraja na wametinga nafasi ya 10 wakitokea ya 13 kwa kufikisha alama 22, lakini bado inaona haipo salama kwa sasa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Razak Rajab, alisema licha ya kujitahidi kupata matokeo mazuri katika mzunguko huu wa pili baada ya kupata sare tatu, kufungwa mchezo mmoja na kushinda mchezo mmoja, lakini bado wanahitaji kupata matokeo mazuri katika michezo iliyosalia ili kuhakikisha timu hiyo haishuki daraja.

Alisema ingawa wametoka katika mstari wa hatari wa kushuka daraja baada ya kukamilika mzunguko wa 20, lakini timu hiyo bado ipo katika hatari kwa kuwa timu zilizopo chini yao zipo nyuma kwa mchezo mmoja na wamepishana alama moja na nyingine alama mbili tu.

Rajab alisema wanahitaji kushinda michezo mingi zaidi na kupata alama ambazo zitawatoa kabisa katika nafasi ya kushuka daraja. "Mzunguko wa kwanza wachezaji wamejitahidi, hawakufanya vibaya sana, kutokana na ushindani wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kucheza michezo hii mitano," alisema.

Aidha, aliwapongeza wachezaji wake kwa kucheza vizuri na kwa mipango kama vile timu inavyohitaji licha ya ugumu wa ligi hiyo hasa mzunguko huu wa lala salama.

Hata hivyo, alisema wataendelea kujipanga kama kawaida ili kujiandaa na michezo ya Kombe la FA japo mipango yao hawakuielekezea sana katika michuano hiyo.




# Stara sasa yaja na 2024 'Kiafrika Zaidi'

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Stara Tanzania inayoratibu Jukwaa la Stara Fashion Week, imezindua kampeni yao mpya kwa mwaka huu kama 2024 Kiafrika Zaidi (Afrocentric).

Kauli mbiu hiyo inalenga kuhimiza Waafrika kurejea katika misingi ya tamaduni zao za asili na kusimamia katika itikadi ya kupenda na kutetea vyakwao dhidi ya tamaduni za kigeni huku ikiwahamasisha kurudisha thamani ya Afrika kwa kukumbatia Uafrika wao.

Taasisi hiyo ambayo inaadhimisha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, imejikita katika kuwasaidia wabunifu na wajasiriamali kwa kuandaa warsha na matamasha mbalimbali ya uwezeshaji.

Kupitia jukwaa hilo wabunifu na wajasiriamali wamefaidika na wiki ya maonesho ya kazi za kiubunifu na ujasiriamali kupitia Stara Fashion Week ambayo huchukua nafasi yake mara moja kwa mwaka.

Akizungumza katika uzinduzi wa jukwaa hilo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mwanzilishi wa jukwaa hilo, Latifah Makau Shehoza, alisema kaulimbiu ya mwaka huu ni Afrocentric, Uafriikanishaji.

Alisema "Uafrikanishaji" ni histilahi iliyowahi kutumiwa na Mwalimu Julius Nyerere (RAI Na. 637) yenye kudokeza dhana ya kitendo au hali ya kukifanya au kukigeuza kitu au hali iwe katika mtazamo wa Kiafrika.

"Pamoja na fasili hiyo ikimaanisha pia jitihada zote zifanywazo, ziwe za kivitendo au kinadharia au kimaadili kuwarudisha Waafrika katika tamaduni zao za asili.

"Kaulimbiu yetu hii kwa mwaka 2024, inakuja kuhamasisha na kuchochea kumkomboa Mwafrika dhidi ya uharamia wa tamaduni za kigeni na mmomonyoko wa maadili, dhidi ya dhana potofu, tukilenga kujistiri na mengi mabaya na machafu yanayotutoa katika Uafrika wetu," alisema.

## ZISIKUPITE

### GALLAGHER ANATAKA KUBAKI

KIUNGO wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher, anataka kubakia Stamford Bridge. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 24, amebakiza miezi 18 katika mkataba wake na amekuwa akihusishwa na kuhamia Tottenham Hotspur. ***(Sky Sports)***

### FERGUSON AFUATILIWA ARSENAL

ARSENAL inamfuatilia mshambuliaji wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 19, huku wakipania kuimarisha safu yao ya ushambuliaji msimu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### AGUERO RUKSA KUCHEZA

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester City, Sergio Aguero, anaweza kurejea kwenye soka. Muargentina huyo mwenye umri wa miaka 35, alistaafu mnamo Desemba 2021 alipopatwa na tatizo la moyo akiichezea Barcelona, lakini daktari wake wa moyo anasema sasa anaweza kucheza tena. ***(Mundo Deportivo)***

### OSIMHEN AWINDWA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Napoli, Victor Osimhen, anaweza kuwa chaguo kwa Arsenal, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Chelsea na Paris St-Germain katika kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Nigeria mwenye umri wa miaka 25. ***(GiveMeSport)***

### HARRISON MKATABA WA KUDUMU

KIUNGO wa kati wa England, Jack Harrison mwenye umri wa miaka 27, anataka kubadilisha uhamisho wake wa mkopo kutoka Leeds United hadi Everton kuwa wa kudumu msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### MFUMO MPYA UNITED

MWEKEZAJI mpya wa Manchester United, Sir Jim Ratcliffe, anataka mfumo mpya wa malipo utambulishwe katika klabu hiyo, huku mishahara ya wachezaji ikitegemea zaidi mafanikio. ***(Mirror)***

### ARSENAL KUSAJILI FOWADI

MKURUGENZI wa Michezo wa Arsenal, Edu, amesema klabu hiyo „tayari ina malengo yetu" alipoulizwa kuhusu ‚Washikabunduki' hao kusajili mshambuliaji mpya. ***(TNT Sports, via Standard)***

### KIKOSI KUREKEBISHWA

KLABU ya Manchester United inalenga kusajili mshambuliaji, mabeki wawili wakati wa marekebisho ya kikosi hicho cha Old Trafford majira ya joto. ***(Telegraph)***

### YILDIZ ATAKIWA JUVE

JUVENTUS imeweka bei ya pauni milioni 51 kumnunua Kenan Yildiz anayewindwa na Arsenal. Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 18, amecheza mechi 15 pekee akiwa na Juventus tangu ajiunge na klabu hiyo akitokea Bayern Munich mwaka wa 2022. ***(Sun)***

### ENDRICK KUTUA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Endrick anatazamiwa kujiunga na Real Madrid atakapofikisha umri wa miaka 18 Julai, lakini Palmeiras wanajaribu kumbakisha hadi Desemba mwaka huu. ***(ESPN)***

## DON ... A SOKA MAG ... A ULAYA




# VAN DIJK SIFA ZOTE KWA KIPA WA LIVER

Pengine mimi ni mmoja wa mashabiki, nimekuwa nikisema ana kiwango cha dunia na...

**LONDON, England**

NAHODHA wa Liverpool, Virgl van Dijk, amemsifu Caoimhin Kelleher kwa kuonesha "kiwango cha dunia" baada ya 'Wekundu' hao kunyakua Kombe la Carabao 2024 pale kwenye dimba la Wembley, Jumapili.

Golikipa huyo wa Ireland ameanza kipindi chote cha mbio za Carabao msimu huu na baada ya kuwazuia Chelsea kwa mikwaju ya penalti katika fainali ya mwaka 2022, kwa mara nyingine tena alionesha kiwango kikubwa kuwaweka pembeni 'The Blues' hao na kuipa Liverpool msingi wa kushinda taji hilo.

Van Dijk alifunga bao la ushindi dakika ya 118, lakini aliamua kuonesha shukrani zake kwa Kelleher, ambaye aliokoa hatari tisa kwenye mchezo huo.

Kipa huyo mwenye kwa hakika alionekana kuwa ndio mchezaji bora wa Liverpool.

"Pengine mimi ni mmoja wa mashabiki wake wakubwa," alisema Van Dijk akiiambia Sky Sports.

"Nimekuwa nikisema kwamba yeye ni wa kiwango cha dunia na aliongezeka tena leo (juzi). Ni kijana mzuri, kipa mzuri, na hilo ndilo tunalohitaji katika klabu kama Liverpool."

Katika mahojiano tofauti ya Sky Sports, Kocha Jurgen Klopp alisema: "Hawakuamini kiwango cha Caoimhin. Uchezaji uliokomaa kama huu. Nasema mara nyingi - tuna kipa bora zaidi duniani (Alisson) na namba mbili bora zaidi duniani."

Akiwa na miaka 25, Kelleher alikuwa miongoni mwa wachezaji wakubwa wa Liverpool. Majeraha yalikuwa yamemaliza sana kikosi cha Klopp na Bobby Clark mwenye miaka 19, James McConnell (19), Jayden Danns (18) na Jarell Quansah miaka 21, wote walikuwa uwanjani. Conor Bradley na Harvey Elliott, wote miaka 20, pia walikuwa wameanza kwenye fainali hiyo.

"Unapokuwa mdogo na kupata fursa, unapaswa kuichukua kwa mikono miwili. Ni wazi kuwa ni rahisi kusema kuliko kufanya, lakini vijana walifanya hivyo," alieleza Van Dijk.

"Utamaduni wa klabu unawafanya wafanye hivyo pia na ni vizuri kuona. Inapaswa kuwa kama mwanzo na wanapaswa kuutumia kuanza. Nina uhakika watafanya hivyo. Ni wazi, wachezaji wakubwa zaidi watarejea kwa wakati, lakini wanapaswa kuendelea kusukuma ili kuwa karibu na timu na kuwa sehemu ya kikosi. Kupitia haya kama kijana wa miaka 17, 18, 19 kunanufaisha tu."

# EDU ASEMA ARSENAL ITASAJILI STRAIKA MPYA

**LONDON, England**

MKURUGENZI wa Michezo wa Arsenal, Edu, amekiri kwamba "anaelewa" kwa nini mashabiki wanaitaka timu kusajili mshambuliaji katika dirisha la usajili la majira ya joto, lakini alitoa maoni machache kuhusu mipango halisi ya klabu hiyo.

Gabriel Jesus alisajiliwa kwa pauni milioni 45 mwaka 2022, lakini ametumia muda mwingi kuwa majeruhi tangu wakati huo, na pia kukiri kwamba hana uwezo mkubwa sana wa kufunga mabao.

Eddie Nketiah ndiye mshambuliaji mwingine pekee wa kati kikosini, lakini hajaanza mara kwa mara tangu Novemba mwaka jana.

Badala yake, Kocha Mikel Arteta amependelea kutumia mawinga waliobadilishwa au washambuliaji wa kati katika nafasi ya 'namba tisa' kama vile Leandro Trossard na Kai Havertz.

"Ninaelewa mashabiki wanachoomba, lakini tayari tuna mawazo yetu na shabaha zetu. Tunapanga mengi kabla ya yale tutakayokabiliana nayo," alisema Edu akiiambia TNT Sports.

"Nitakuwa na wasiwasi ikiwa hatufungi mabao mengi, ikiwa hatutengenezi nafasi, ambayo ni kinyume, nadhani tunatengeneza sana, tunafunga mabao mengi. Mpango ni kwa kila mwaka kujaribu kuwa bora, nadhani tuko katika wakati mzuri na tuone kama tunaweza kuendelea kuboresha."



Mabao ya Arsenal ya msimu uliopita yalikuwa shirikishi kupitia kwa Bukayo Saka, Martin Odegaard na Gabriel Martinelli wote wakisajili 15 katika mashindano yote.

Saka ana mabao 16 hadi sasa msimu huu wa 2023/24, lakini hakuna mchezaji aliyevuka mabao 20 kwa msimu mmoja tangu Pierre-Emerick Aubameyang afunge 29 msimu wa 2019/20.

90min inaelewa kwamba Arsenal inamfuatilia mshambuliaji wa Uholanzi wa chini ya miaka 21 wa Bologna, Joshua Zirkzee, kama vile Manchester United. Nia pia imeoneshwa kwa Dusan Vlahovic, wakati mazungumzo yalifanyika na wawakilishi wa Ivan Toney, lakini walikutana na bei mbaya kutoka kwa Brentford.

## Ancelotti: Modric ataamua mwenyewe

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti amekiri kwamba ni „vigumu" kumuacha Luka Modric kwenye benchi baada ya kiungo huyo mkongwe kufunga bao zuri katika ushindi wa 1-0 wa Real Madrid kwenye LaLiga dhidi ya Sevilla Jumapili.

Modric mwenye umri wa miaka 38 - ambaye ameanza mechi 11 pekee za ligi msimu huu – aliingizwa kutoka benchi katika dakika ya 75 kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu na akafunga bao kwa shuti la mbali dakika sita tu baada ya kuingia.

Mkataba wa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Croatia unatarajiwa kumalizika msimu huu wa majira ya joto, na kukosa muda wa kucheza msimu huu kumesababisha uvumi kuwa anaweza kuchagua kuhama baada ya miaka 12 ya kukaa na Madrid.

"Modric alistahili leo (juzi),“ alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Alifunga bao zuri. Alichangia sana alipoingia, alileta hali mpya.

"Ni vigumu kumuacha kwenye benchi. Jinsi anavyofanya mazoezi kila siku, ni mfano kwa kikosi kizima.“

Ancelotti alisema kuwa Modric - pamoja na Toni Kroos na Nacho Fernandez, ambao mikataba yao pia inakamilika msimu huu wa majira ya joto - wamepata haki ya kuamua mustakabali wao wenyewe.

"Modric, Kroos, Nacho wote wako katika hali moja,“ alisema Ancelotti. "Siingii katika hilo. Klabu ina muda wa kutatua hayo yote miezi michache ijayo...kutokana na heshima niliyonayo kwa Modric siwezi kumpa ushauri, ana akili sana, anajua vizuri kabisa kile anachopaswa kufanya."

Modric ameshinda mataji 24 akiwa na Madrid yakiwamo matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini anakabiliwa na ushindani ulioongezeka katika safu ya kiungo msimu huu kutoka kwa vijana Jude Bellingham, Eduardo Camavinga, Fede Valverde na Aurelien Tchouameni, pamoja na Kroos, ambaye amekuwa katika kiwango bora.




## Barca haiwauzi De Jong, Araujo

**BARCELONA, Hispania**

MKURUGENZI wa Michezo wa Barcelona, Deco, amekanusha uwezekano wa klabu hiyo kumuuza Frenkie de Jong au Ronald Araujo katika dirisha la usajili la majira ya joto.

De Jong pia kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa kuuzwa, huku uvumi wa hivi majuzi zaidi ukiegemea juu ya madai ya Paris Saint-Germain kumtaka.

Araujo amekuwa akilengwa na Bayern Munich katika miezi ya hivi karibuni, na pia kuhusishwa na Manchester United.

"Hakuna kitakachofanyika," alisema Deco akiiambia Movistar alipoulizwa kuhusu wawili hao.

"Wana mkataba na tunataka kuweka ubora zaidi. Na ni bora zaidi. Ni wachezaji ambao wamepata haki ya kuwa Barca na wamepata heshima ya mashabiki na klabu. Tunataka kuendelea kuwategemea."

Araujo aliongeza muda wake 2022 kwa mkataba wake wa sasa ambao utaendelea hadi 2026, pamoja na kifungu cha kuuzwa cha euro bilioni moja. Mkataba wa De Jong pia unamalizika 2026. Deco amepotiwa kukutana na mchezaji huyo na wakala wake ili kuwahakikishia kuwa Barca hawako nyuma ya uvumi unaodaiwa kwamba hana furaha.



Maofisa wa Barca wamelazimika kufanya kwa bidii zaidi katika miaka ya hivi karibuni ili kuirejesha klabu hiyo kutoka kwenye ukingo wa kusahaulika kifedha. Mikataba imepunguzwa mara kwa mara na wachezaji wengi kuuzwa ili kupunguza gharama.

Dili lilikubaliwa hata kumuuza De Jong kwenda Manchester United msimu wa majira ya joto wa 2022 hadi mchezaji huyo alikataa na uhamisho huo ukashindikana.

Lakini Rais Joan Laporta alidai mapema mwezi huu kwamba mwanga unaonekana mwishoni mwa handaki hilo.

"Ikiwa tutafikia bajeti, zama za giza zaidi katika historia ya FC Barcelona zitaisha," alisema.

"Bajeti inazalisha ziada bila kuuza mali. Klabu imekuwa ikifanya kazi nzuri hapa. Gharama na deni zimepungua kwa zaidi ya miaka miwili. Hii imetokana na mauzo makubwa yaliyotokana na kupunguza mishahara ya michezo."

# TWIGA STARS NI KUFA KUPONA KWA BANYANA BANYANA LEO

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tanzania ya Wanawake, Twiga Stars, leo inashuka dimbani nchini Afrika Kusini dhidi ya Banyana Banyana ikiwa na lengo moja tu, kucheza kufa kupona ili kupindua matokeo ya mabao 3-0 waliyoruhusu katika mechi ya awali hapa nchini na kuweka matumaini yao hai ya kufuzu michuano ya Olimpiki.

Kuelekea mchezo huo Kocha wa Twiga Stars, Bakari Shime, amesema hautakuwa rahisi na mambo mawili wameyafanyia kazi ambayo ni ubora na udhaifu wa wapinzani wao, lengo likiwa ni kuyatumia kupata matokeo mazuri.

Alisema licha ya kupoteza nyumbani kwa mabao 3-0, vijana wake hawajakata tamaa na wanaonyesha ari ya kupambana kuweza kupata matokeo ya idadi ya mabao ambayo wapinzani wao walipata.

"Maandalizi tulishafanya tangu nyumbani na tumeandaa mipango na mikakati yetu kuelekea mchezo wetu wa kesho (leo), wachezaji hawajakata tamaa, hii inanipa matumaini ya kufanya vizuri katika mchezo wetu.

„Hautakuwa mchezo rahisi kama nilivyosema awali kulingana na ubora wa wapinzani wetu, lakini morali ya vijana wangu inanipa matumaini ya kupambana na kuweza kupata matokeo," alisema Shime.



Wafanyakazi wa Benki ya Azania wakiongozwa na Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani, Oswald Matilya (wa pili kushoto mwenye kofia), wakiwa na nyuso za furaha baada ya kumaliza mbio za Kili Marathon 2024 zilizofanyika juzi mjini Moshi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Crissa aweka rekodi kuogelea

**Na Shufaa Lyimo**

MUOGELEAJI wa Klabu ya Taliss, Crissa Dillip, ameweka rekodi kwenye mashindano ya Kuogelea ya Vijana, Taliss IST, baada ya kuibuka na medali saba za dhahabu pamoja na kombe.

Mashindano hayo yalimalizika juzi kwenye Bwawa la kuogelea la IST, Masaki jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe baada ya mashindano hayo, Dillip alisema siri ya mafanikio yake hayo imetokana na mazoezi ya muda mrefu aliyofanya pamoja na kufuata vema maelekezo anayopewa na kocha wake.

"Nimepata medali nyingi kwa sababu nina juhudi ya kufanya mazoezi pamoja na kufuata maelekezo ninayopewa na kocha wangu," alisema Dillip.

Alisema mashindano yalikuwa na upinzani mkubwa kwani kila klabu ilionyesha kiwango kizuri na kuwataka wasichana wajifunze mchezo wa kuogelea kwa kuwa ni miongoni mwa michezo bora inayozidi kukua hapa nchini.

Dillip alisema malengo yake ni kufanya vizuri zaidi kwenye mashindano mbalimbali ya kimataifa ili kupeperusha vema bendera ya Tanzania.

Kwa upande wa Meneja wa klabu hiyo, Hadija Sheba, aliwapongeza washindi wote pamoja na kuwashukuru wazazi waliowaruhusu watoto wao kushiriki michuano hiyo.

Mashindano hayo yalishirikisha klabu kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar, pamoja na timu moja kutoka Nairobi nchini Kenya.



Kinara wa kuogelea, Crissa Dillip akiwa na medali za dhahabu pamoja na Kombe baada ya kushinda kwenye mashindano ya Taliss IST juzi kwenye bwawa la IST Masaki, Dar es Salaam.

## Benchikha achora ramani ya kuimaliza

INATOKA UK. 24

kisasi," alisema nahodha huyo.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema mechi dhidi ya Jwaneng Galaxy itachezwa Jumamosi saa 1:00 usiku, kwa sababu ya maelekezo ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kutaka ipigwe muda huo sawa na ile Wydad Casablanca dhidi ya Asec Mimosas.

Alisema kikosi kimerejea nyumbani na kinaingia kambini moja kwa moja kuendelea na maandalizi ya kujiandaa na mchezo wa Kombe la Shirikisho Soka nchini, maarufu FA Cup dhidi ya TRA utakaochezwa keshokutwa, Jumatano.

"Timu imerejea na kuingia kambini kujiandaa na mchezo huo pamoja na mechi ya kimataifa dhidi ya Jwaneng Galaxy ambao tutacheza Machi 2, mwaka huu, bado hatujapata taarifa ya lini wapinzani wetu wanakuja licha ya baadhi ya watu wao kufika nchini.

"Huu ni mchezo muhimu sana kushinda, kutafuta ushindi wa aina yoyote, hatusubiri kuangalia mechi ya Wydad Casablanca dhidi ya Asec Mimosas. Kama tukishinda tunatimiza alama tisa hali kadhalika Wydad wakishinda wanakuwa na pointi sawa na sisi.

"Lakini Simba itaenda kwa sababu ya kanuni kwa kuwa tulipokutana na Wydad Casablanca walitufunga kwao bao 1-0 na walipokuja hapa tukawafunga mabao 2-0 hiyo itatufanya twende kwa mara ya tano robo fainali," alisema Ahmed.

Alisema kila Mwanasimba aliyefanikiwa kuifanya timu yao kuvuna alama sita katika makundi, sasa wajitokeze kwa wingi Jumamosi uwanjani kuhakikisha wanatinga hatua ya robo fainali kwa mara ya tano.

"Hii Jwaneng Galaxy tunaikumbuka sana 2021, walitusababishia maumivu makubwa ambayo hayajasahaulika kwa Wanasimba, sasa wamekuja kwetu tumejipanga kulipa kisasi kwa siku ya Machi 2, huu ni muda wa wao kuwapa mateso," alisema.

Alieleza kuwa safari hii katika mchezo huo una mambo mawili kwanza ni kutafuta ushindi na pili kulipa kisasi kwa Jwaneng Galaxy, na kwamba hamasa kuelekea mechi hiyo itaanza kesho, Jumatano eneo la Keko, wilayani Temeke, Dar es Salaam.

"Mgeni rasmi wa mchezo wetu ni beki, Henock Inonga, ambaye ni mchezaji pekee ameipeleka timu yake ya taifa kucheza mshindi wa nne wa michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon)," alisema Ahmed.

Kuhusu waamuzi wa mchezo huo alisema wanatarajia kutumia nchini Februari 29, mwaka huu, wakitokea nchini Ghana, ambao ni Daniel Jim Ayi Laryee, Kwasi Acheampony Brobbey, Roland Nii Dondoo Addy na Charles Banle Bulu.

Ahmed pia alitangaza viingilio vya mchezo huo kuwa mzunguko ni Sh. 5,000, VIP C Sh. 10,000, VIP B Sh. 20,000, VIP A Sh. 30,000, Platinum Sh. 150,000 na safari hii kuna tiketi za Tanzanite ambazo ni Sh. 200,000, hizo zikiwa ni kwa watu maalum ambao watakaa karibuni na viongozi watakaojitokeza uwanjani.

Michezo
Jumanne Februari 27, 2024
Nipashe

Van Dijk sifa zote kwa kipa wa Liver UKURASA 21



# BENCHIKHA ACHORA RAMANI YA KUIMALIZA JWANENG



●●●Waunganisha kambini, Inonga mgeni rasmi, waamuzi Waghana kuamua, kuziona buku 5...

**Na Saada Akida**

BAADA ya Simba kuwasili nchini jana ikitokea Ivory Coast, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdelhak Benchikha, tayari amechora ramani yake kuelekea mchezo ujao wa mwisho wa hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo moja kwa moja amewataka wachezaji wake kuelekea kambini kuanza maandalizi ya mtanange huo.

Simba ambayo mchezo uliopita dhidi ya Asec Mimosas, ilitoka suluhu, sasa inahitaji ushindi wa aina yoyote Jumamosi wiki itakapoikaribisha Jwaneng Galaxy ya Botswana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.



Inonga

Akizungumza na Nipashe jana, Benchikha alisema hii ni mechi muhimu sana kushinda na kwenda hatua ya robo fainali, hivyo lazima wapambane na kutafuta matokeo mazuri uwanja wa nyumbani.

Alisema kubwa kwake ni kufanyia kazi nafasi wanazozipata na kushindwa kuzibadili kuwa mabao, hususan kuelekea mchezo huo muhimu ambao wanahitaji ushindi ili kufuzu robo fainali ya michuano hiyo kwa mara nyingine.

Benchikha alisema mechi yao na Asec Mimosas walicheza vizuri sana, lakini walishindwa kutumia nafasi iliyopatikana kupitia kwa Sadio Kanoute, ambayo ingekuwa muhimu sana kwao.

"Tunasahau hilo, tumerejea nyumbani kusahihisha makosa yetu, kundi ni gumu sana, lakini kwetu tunataka kushinda mechi yetu ya Jwaneng Galaxy kwa sababu itatuwezesha kufuzu kucheza robo fainali kwa mara nyingine.

"Tunajua historia ya wapinzani wetu miaka ya nyuma, lakini haihitaji kuiweka akili zaidi ya kuandaa timu na wachezaji kutumia nafasi wanazotengeneza kutafuta ushindi," alisema Benchikha.

Nahodha wa Simba, Mohammed Hussein, alisema wamerejea nyumbani na wanaingia kwenye mechi dhidi ya Jwaneng Galaxy kwa tahadhari kubwa kulingana na kuwafahamu wapinzani wao hao.

"Hii ni mechi ngumu sana na muhimu kwa Wanasimba wote kujitokeza uwanjani kwa sababu inatoa hatima yetu ya kwenda kucheza robo fainali kwa mara nyingine.

"Tunawakumbuka sana Jwaneng Galaxy kwa kilichotokea Uwanja wa Benjamin Mkapa 2021, hatutafanya makosa tena na tunahitaji kushinda mechi hii ambayo itatupeleka hatua ya robo fainali, lakini tunataka kulipa

INAENDELEA UK. 23

# Guede aahidi moto zaidi Yanga

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Joseph Guede, amesema amefurahi kushusha presha yake na ya mashabiki pia baada ya kufunga bao, hivyo kuahidi kufanya vizuri na kukata kiu yao katika suala la kufunga.

Guede aliyepachika bao la nne katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Jumamosi iliyopita dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria na kuipeleka timu hiyo hatua ya robo fainali kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ikishinda mabao 4-0, amesema kwa sasa yeye na mashabiki pia hawana presha kama ilivyokuwa mwanzo, kwani yeye alikuwa anataka kufunga ili kuonyesha kama ana uwezo huo, na mashabiki walikuwa na wasiwasi naye kama anaweza kufanya hivyo.

Amewaambia waandishi wetu kuwa kwa sasa anaimani mashabiki wa Yanga pamoja na kwamba wanataka kuona anafanya vizuri kwa kufunga katika mechi mbalimbali, lakini hawatokuwa na presha sana kama ilivyokuwa mwanzo kabla hajafunga bao.


"Ilikuwa ni ngumu mchezaji kuingia moja kwa moja kwenye timu na kufanya vizuri, nimepata muda na sasa niko vizuri kuhakikisha nakata kiu ya wanachama na mashabiki ambao wanataka kuona nafunga kwa kila mechi," alisema Guede.

Aliongeza kuwa kwa sasa atapambana kila anapopewa nafasi ya kucheza kwa ajili ya kuwapa furaha mashabiki wa Yanga akiamini atafunga anapopata nafasi ndani ya timu hiyo kwani hatokuwa na wasiwasi tena kwa sababu hata ikitokea akapoteza nafasi mashabiki hawatomchukulia kama walivyokuwa wakimchukulia awali.

Wakati huo huo nahodha wa timu hiyo, Bakari Mwamnyeto, amesema wanakwenda kucheza mechi ya mwisho dhidi ya Mabingwa Watetezi, Al Ahly ya Misri bila presha, hivyo wanaweza pia kuweka rekodi nyingine katika bara la Afrika.

Mwamnyeto alisema awali walikuwa na wasiwasi na mechi hiyo kwa sababu walidhani watakwenda kucheza kwa ajili ya kusaka matokeo, lakini kwa sababu wameshapita, ikiwamo wenyeji wao, wanaweza pia kuweka rekodi ya kuifunga Al Ahly nyumbani kwao kwa mara ya kwanza kwenye historia ya Yanga.

"Mpira ndivyo ulivyo, nani alijua kama tutaifunga CR Belouizdad mabao 4-0, hivi sasa tunamuachia kocha wetu, apange mipango yake na kutupa maelekezo ya jinsi ya kucheza nao, mfumo upi, tucheze vipi, lakini nakuhakikishia patachimbika, mpira utapigwa kwa sababu tutacheza bila presha," alisema nahodha huyo.



Guede

Yanga itamaliza mechi yake ya sita Kundi D dhidi ya Al Ahly jijini Cairo, Ijumaa ijayo katika mechi ambayo itaamua timu gani itashika nafasi ya kwanza na ya pili.

Wakati Al Ahly ina pointi tisa, ikiwa kileleni Yanga ina pointi nane, ikiwa nafasi ya pili. Kila mshindi wa kwanza wa kundi atacheza mechi ya robo fainali na mshindi wa pili wa makundi mengine na kuanzia ugenini, huku watakaoshika nafasi ya pili watakumbana na vinara wa makundi ambapo wataanzia nyumbani na kumalizika mechi zao ugenini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >